# *Ni Mimi Msiogope*

Asante, Ndugu Borders.

2 Mwaweza kuketi. Ninahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu usiku wa leo, kuwa katika nyumba ya Mungu kuwahudumia watoto Wake wagonjwa. Nasi tunasikitika kwamba hatuna nafasi nzuri ya kuketi—ya kuketi kwa ajili yenu. Tulipokuwa tukija barabarani kulikuwako na magari matatu ama manne yakiondoka, halafu, tukaja *huku*, na kulikuwako na mlolongo wa watu waliokuwa wakiondoka kanisani, kwamba hawakuwa na nafasi ya kuingia. Na labda kufikia Jumapili ijayo, kama tutajaribu sana, labda tungeweza kupata jumba la mikutano kwa ajili ya usiku wa kumalizia hapa chini, na tungeweza kumwingiza kila mtu.

3 Unapokuwa na umati uliosongamana, ina—inafikia mahali ambapo inawafanya watu washikwe na wasiwasi, na unapowafanya wasikilizaji kuwa na wasiwasi, Roho Mtakatifu hawezi kufanya kazi. Inakubidi kumjia Mungu tu kwa kicho, kwa utulivu, ukiamini, bila usumbufu wowote, ndipo Roho Mtakatifu, ni rahisi zaidi Kwake kutushughulikia.

4 Hakika tulikuwa na wakati mzuri sana juma hili hapa kanisani, wamekuwa wakizungumza juu ya ibada, juu ya masomo ya Ibrahimu, wakijenga imani kwa ajili ya usiku wa leo, kwa ajili ya ibada ya uponyaji. Tumegeuza sehemu hii ya ibada kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa.

5 Sasa, ningetaka kila mtu ashike Neno la Mungu kwanza, kwa sababu uponyaji ni wa Mungu . . . uko katika upatanisho. Kama ule upatanisho wa kale ulileta uponyaji, huu ni Upatanisho bora zaidi, bila shaka ungekuwa na uponyaji ndani yake. Nayo Biblia ilisema, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

6 Sasa, uponyaji hauko ndani ya mwanadamu. Sasa, uponyaji ni—ni baraka ya ukombozi wa Mungu ambayo tayari imenunuliwa kwa ajili yako pale Kalvari. Wokovu si kitu kinachotukia usiku wa leo, wokovu wako ulinunuliwa miaka elfu moja mia tisa iliyopita wakati Kristo alipokufa kwa ajili yako pale Kalvari, Yeye . . . hapo ndipo wokovu wako uliponunuliwa.

7 Sasa, huna budi kulikubali kwa ajili ya mambo yako binafsi. Unasema, "Mimi ni mwenye dhambi na Kristo alikufa kwa ajili yangu, na mimi ndiye ambaye Yeye alikufia, kwa hiyo basi, usiku wa leo, ninakuja juu ya msingi wa Damu iliyomwagika, nami ninaukubali wokovu wangu, nikijua hakuna kitu ninachoweza kufanya mwenyewe, nami ninamtumainia kabisa na kikamilifu usiku wa leo, na kuamini ya kwamba Yeye

ananiokoa, kulingana na ahadi Yake," basi umeokoka, haidhuru kama una mhemuko, ama huna mhemko, unaokolewa kwa imani katika kazi iliyomalizika pale Kalvari.

8 Sasa, hivyo ndivyo unavyoponywa. Wakati wewe... Sasa, unasema, "Vema, basi, hata haingenibidi kuja kanisani nipate kuokolewa." Hiyo ni kweli. Mahali popote unapotimiza matakwa ya Mungu, hapo ndipo unapookolewa; mahali popote unapotimiza matakwa ya Mungu, hapo ndipo unapoponyewa.

9 Sasa, Mungu hawezi kubadilisha maoni Yake juu ya mambo. Daima tunasema jambo hilo, ya kwamba ninii yetu... tunaiwekea msingi imani yetu kwa dhati juu ya Neno la Bwana, kwa kuwa Mungu anaposema jambo lolote, hawezi kulighairi. Yeye ni Mungu, Yeye hana kikomo, kila uamuzi ni mkamilifu.

10 Na sasa, kama alifanya uamuzi Wake *hapa*, na ni mkamilifu, sasa, Yeye hawezi kufanya uamuzi mkamilifu zaidi katika wakati mwingine, hana budi kufanya uamuzi ule ule, kwa sababu, kama angefanya hivyo, angepungukiwa na kile alichokuwa nacho katika *huu*. Na kama alifanya uamuzi mbaya *hapo*, vema, basi kama alifanya uamuzi tofauti, hasa, *hapa* tofauti na alivyofanya *hapa*, basi alikosea *hapa*. Na kama alikosea, basi asingeweza kuwa ni Mungu. Mnaona? Kwa hiyo, lazima mkumbuke wakati Bwana anaposema jambo lolote, hivyo ndivyo litakavyokuwa hasa.

11 Na sasa, wewe mwenyewe...Sasa, mara nyingi nimeona watu wakinyakua imani, na kujaribu kuifikia, mara nyingi watu wanapita juu yake. Imani ni rahisi sana. Ni kwamba tu, katika Biblia mliona kile walichotumia kupaka damu? Kilikuwa hisopo. Vema, hisopo ni magugu tu ya kawaida, na huko chini Misri, na pia huko Palestina unaiona ikikulia kwenye nyufa za matofali, na kadhalika, moja kwa moja ardhini, jani dogo tu la kijani kibichi, lenye umbo la pembe tatu, lenye umbo la almasi na ua dogo juu yake, ungeweza tu kuliokota popote, ilikuwa ni hisopo. Hiyo ndiyo waliyopaka damu nayo kwenye kizingiti cha mlango, hisopo. Na sababu yake, waliifanya magugu kwa sababu inawakilisha imani.

12 Unapakaje Damu? Kwa imani, si kitu fulani kikuu, bali imani tu ya kawaida, kama uliyo nayo, hivyo ndivyo unavyopaka Damu. Kama vile, unasema, "Ninatoka kwenda kuingia kwenye gari langu, niende nyumbani." Unajuaje unaenda? Huna hakika na jambo hilo, karibu una hakika nalo, bali unaamini una hakika, basi endelea tu, ukitenda, na uendelee.

13 Hivyo ndivyo uponyaji ulivyo. Mwamini tu Bwana Yesu Kristo, mkubali Yeye kama Mponyaji wako juu ya msingi wa Damu Yake iliyomwagika, kwamba alijeruhiwa kwa makosa yako, kwa kupigwa Kwake wewe uliponywa, si *utaponywa* bali *uliponywa*, wakati uliopita. Tayari umeponywa kwa kupigwa

Kwake. Nafikiri hilo ndilo jambo la ajabu sana, "Kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*," katika wakati uliopita, "tuliponywa."

14 Sasa, Bw. Roberts, Bw. Tommy Osborn, Bw. A. A. Allen, loo, wengi sana wa hao ndugu hudumani walio na huduma ya kuwawekea wagonjwa mikono na kuwaombea (Na hapo ndipo ninapopata *mahali pa kurudia*, "Huwaombei wa kutosha.") sasa, hao ndugu Wakristo, ninaamini ya kwamba wana huduma kutoka kwa Mungu. Na sasa, wanawaombea mamia na mamia kila usiku. Sasa, hiyo labda . . . Sasa, ninaamini kwa moyo wangu wote kwamba wanafanya yale Mungu aliyowaambia wafanye, hiyo ndiyo huduma yao.

15 Sasa, lakini kama mtanivumilia tu kwa dakika moja, ninaamini kuna njia ya juu zaidi ya kumfikia Kristo kuliko kuwekea mikono, maana, kama ukiangalia, mgonjwa anaweza kusema hivi: "Ndugu *Nanii* aliniwekea mikono, nilihisi nguvu za Mungu zikija kupitia mikononi mwake," mnaona, hilo linamweka mtu ndani yake tena, mnaona.

16 Lakini hayo yalikuwa ni mapokeo ya Kiyahudi. Kama mkiangalia, maskini kuhani huyo alisema, "Njoo uweke mikono yako juu ya binti yangu," Yairo, "naye atakuwa mzima." Sasa, huyo, alikuwa ni Myahudi.

17 Lakini yule Mrumi, Mmataifa, alisema, "Sistahili Wewe uje chini ya paa langu. Nena tu Neno, na mtumishi wangu ataishi." Mnaona mahali ambapo hiyo imani ya Kirumi . . .? Ilimweka Yesu . . .

18 Akaendelea kusema, "Mimi ni mtu chini ya mamlaka." Alikuwa akida, ambayo inamaanisha alikuwa chini ya karne moja, watu mia moja, katika jeshi la Kirumi. Akasema, "Nikimwambia *huyu*, 'Nenda,' anaenda; na *huyu*, 'Njoo,' anakuja." Alijua ya kwamba kila kitu kilikuwa chini ya mamlaka yake alichokuwa amedhibiti, ilibidi kimtii. Alisema nini, basi, wakati alipomkiri Kristo, kwa jambo hilo? "Nikimwambia nanii wangu . . . " Yeye alisema hivi: "Wewe ni . . . Una mamlaka juu ya chochote, juu ya ugonjwa wowote, sema tu Neno."

19 Yesu alisema nini kuhusu hilo? Aligeuka, na bila shaka Yeye—Yeye alimheshimu Mrumi huyo, akasema, "Sijaona imani kama hiyo katika Israeli." Mnaona?

20 "Usije ukamwekea mikono yako, nena tu Neno." Sasa, hapo ndipo tunapojaribu kuwafikisha watu, kuamini ya kwamba Yeye . . . Si mwanadamu fulani, ni Bwana wako, Yesu Kristo, ni yale Yeye aliyokufanyia.

21 Sasa, jambo kuu linaloonekana kuwapata watu siku hizi, ni kwamba wanajaribu kuwazia kwamba tunamtumikia namna fulani ya Mungu wa kihistoria, ama Yeye alikuwa ni Mponyaji mkuu katika siku moja, ama Yeye alikuwa Mtu mkuu katika siku moja, bali siku hizi ni kumbukumbu, jambo la kihistoria. Hilo

ni kosa. Biblia ilisema Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Naye yu hai; kama Yeye angali hai, na kama angali hai, hana budi kuwa yeye yule katika maumbile, yeye yule katika nguvu, yeye yule katika mtazamo. Ni Yesu yeye yule, Waebrania 13:8, yeye yule jana, leo, na hata milele.

22 Kama kungekuwa na njia yoyote ambayo ningeweza, vema basi. . .Mimi si daktari, sijui chochote kuhusu tiba, wala upasuaji. Ni—ninaheshimu na kuamini katika tiba na upasuaji, ninaamini ni baraka zilizotumwa na Mungu kwetu, lakini wakati mwingine tunafikia mahali ambapo ni zaidi ya yale sayansi yetu ya tiba inayoweza—inayoweza kushughulikia, basi inapofikia jambo hilo, nafikiri, badala ya kukata tamaa na kufa, tuna haki ya kumjia Tabibu Mkuu.

23 Kama daktari wako wa mahali hapo asingeweza kukusaidia, una haki ya kwenda kwa mtaalamu, na kama huyo mtaalamu hawezi kukusaidia, basi hebu tumwendee Mtaalamu wa wataalamu, Yesu. Hiyo ndiyo sababu niko hapa, si kumchukua mgonjwa wa daktari, bali kumwombea mgonjwa wa daktari, mtoto wa Mungu, na rafiki yangu, hiyo ndiyo sababu niko hapa.

24 Sasa, dawa haiponyi, sote tunajua hilo, hakuna dawa inayodai kuponya, madaktari hawadai hilo. Dawa ni msaada kwa maumbile, Mungu ndiye Mponyaji. Hakujawahi kuwa na mtu yeyote aliyeponywa kwa dawa, huwezi kumponya. Uponyaji ni kukuzwa kwa tishu, wala hakuna kitu kitakachokuza tishu ila uhai, kukuza tishu.

25 Sasa, tunaweza kuwa na ninii kuu. . .kufanya mambo makuu kwa kuweka mfupa, lakini sasa, hiyo haiuponyi huo mfupa, inaurudisha tu ili Mungu auponye. Kitu fulani hakina budi kutoa kalisi, na kadhalika, kuuponya mfupa huo. Sasa, daktari. . .Ni ninii yako—ni ninii yako. . .Unachopaswa kufanya ni kumwendea daktari na kumwacha auweke, lakini Mungu asipouponya, kamwe hautapona. Una jino bovu, daktari anaweza kuling'oa, bali hawezi kuponya tundu hilo, na tishu alizopasua. Huenda akaondoa kidole tumbo, ama kivimbe ubavuni mwako, ama kitu fulani, bali hawezi kuponya mahali kilipotokea; anaweza kuondoa, lakini hawezi kuponya.

26 Dawa haiponyi, hakuna dawa inayoponya, inadumisha tu safi, wakati Mungu akiponya, nasi hatuna budi kukumbuka hilo.

27 Na sasa, usiku wa leo, tunapomwendea kwa ajili ya uponyaji, sasa, ningetaka kuuliza jambo hili moja, kama. . .Ni watu wangapi hapa ndani ungeinua mkono wako kwa hili, kwamba unaamini ya kwamba Maandiko yanasema, katika Waebrania 13:8, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Asanteni.

28 Basi kama unaamini hilo, kama Maandiko yanasema hivyo, basi huna budi kukumbuka yale Maandiko yanayosema ni kweli. Sasa, Yesu alisema, wakati alipokuwa hapa duniani, ya kwamba

Yeye hakufanya yoyote ya hizo kazi Mwenyewe, sote tunajua hilo, Yeye alisema, "Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu, Yeye huzitenda hizo kazi." Hiyo ni kweli, sivyo?

29 Na katika Yohana 5:19 aliulizwa juu ya kupitia kwenye birika ambako kulikuwa na maelfu ya watu, viwete, vipofu, vilema, na waliopooza, Naye akamwona mtu amelala kwenye godoro, Naye alijua alikuwa katika hali hiyo kwa muda wa miaka thelathini na minane, akamponya, kisha akaondoka, na kuuacha umati huo wa watu umelala pale, ndipo akaulizwa.

30 Nadhani kama Yeye alikuwa katika mwili wa kawaida akitembea miongoni mwetu usiku wa leo, angefanyiwa jambo lile lile, angehojiwa tena na viongozi wetu. Naye akasema maneno haya, sasa, yaweke moyoni mwako, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile *amwonalo* Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile."

31 Sasa, ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli ya Kimaandiko? Basi Yesu kamwe hakufanya miujiza yoyote mpaka Mungu alipomwonyesha kwa ono jambo la kufanya kwanza. Kama sivyo, basi Yeye alisema jambo ambalo halikuwa hivyo, na hilo linayafanya Maandiko kukosea. Basi tuko wapi? Mnaona? Hakufanya hivyo kwa kubahatisha tu, hakuna nabii aliyewahi kufanya hivyo kwa kubahatisha, walifanya tu kama Mungu alivyowaambia na kuwaonyesha la kufanya.

32 Sasa, wakati Yesu alipokuwa duniani, alijitangaza Mwenyewe kuwa Masihi, naye Yohana alitangaza kulikuwako na ishara ya Masihi iliyomfuata, na Agano la Kale lilidai kungekuwako na ishara ya Masihi, Naye akathibitisha ishara hiyo ya Masihi kwa watu, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Jinsi walivyojua jambo hilo, ilikuwa kwamba Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii. Musa, yule waliyekuwa wamemfuata, alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi." Tunajua jambo hilo, tunajua hilo.

33 Na miongoni mwa Wayahudi na—na Wasamaria alionyesha ishara hii, bila shaka, Yeye kamwe hakuionyesha miongoni mwa Mataifa, kwa sababu tulikuwa makafiri siku hizo, watu wetu, Mataifa, Warumi. Hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote, naye Masihi huwatokea tu wale wanaomtazamia. Hivyo ndivyo... Wale wanaomngojea, Yeye atatokea mara ya pili. Kwa hiyo ingetubidi sisi, usiku wa leo, kuwa tukimngojea na kumtazamia, tusije tukamkosa wakati atakapokuja.

34 Sasa, Yesu kabla hajaondoka, ninanukuu Maandiko haya kabla sijagusia ujumbe wangu, Yesu kabla ya kuondoka duniani, Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena." Sasa, *ulimwengu* hapo ni neno *kosmos*, ambalo linamaanisha, "utaratibu wa ulimwengu." Mnaona? "Ulimwengu hautaniona tena, ila, ninyi mtaniona," hilo ni

Kanisa, "kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Sasa, sote tunajua Maandiko yanasema hivyo. Sasa, basi hilo linamfanya Yesu yeye yule jana na hata milele.

35 Sasa angalieni, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, na zaidi," sasa, ninajua toleo la King James linasema *makubwa zaidi*, lakini ukichukua *Tafsiri Asili*. . .Hakuna mtu angaliweza kufanya makubwa zaidi, Yeye aliwafufua wafu, akatuliza maumbile, *nyingi*, kwa sababu wakati huo, Mungu alikuwa katika Mtu mmoja, Kristo Yesu, "Utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake," Maandiko yanasema. Timotheo wa Kwanza 3:16, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu, maana Mungu alidhihirishwa katika mwili."

36 Aliitwa *Imanueli*. Yeye alikuwa katika Mtu mmoja tu, bali Yeye, wakati Yeye, Mtu huyu mmoja, akiwa ni Mwana wa Mungu, aliutoa uhai Wake apate kulitakasa Kanisa Lake apate kurudi katika umbo la Roho Mtakatifu, na awe katika Kanisa Lake, ulimwenguni kote. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," aina ile ile, "*nyingi* kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu," kusudi aweze kurudi katika umbo la Roho Mtakatifu na awe katika Kanisa Lake, ulimwenguni kote.

37 Ni kwa maungamo yangu, usiku wa leo, ya kwamba Yesu Kristo yu hai wala hajafa, Yeye anaishi katika Kanisa Lake. Ingawa nyingi za kanuni zetu za imani zimemsukumia nje, kama Biblia, tunaona katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati wa mwisho wa kanisa, ambao ni wakati wa Kipentekoste tuliomo sasa, Yesu alikuwa amesimama, amefukuzwa kanisani Mwake, akibisha mlango akijaribu kurudi ndani. "Wote niwapendao mimi nawakemea na kuwarudi," nikijaribu, "mtu awaye yote akifungua, nitaingia na kula pamoja naye."

38 Sasa, juu ya jambo hili, juu ya maungamo haya kwamba, kama tunaweza kuona usiku wa leo katika jengo hili ya kwamba Yesu angali hai, na tunaweza kuthibitisha bila shaka ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, katika umbo la Roho Mtakatifu, yuko moja kwa moja katika jengo hili, basi kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Atatenda vile vile kama alivyotenda jana, leo, na hata milele, huruma Zake na upendo vitakuwa vile vile.

39 Nalo lilijengwa juu ya msingi wa, "Kama unaweza kuamini, ninaweza. Ninafanya vile Baba anavyonionyesha." Kama vile yule mwanamke alivyogusa vazi Lake, nguvu zikatoka. Aliangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akamwona yule mwanamke aliyemgusa, Akasema, akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu kumekoma kwa sababu imani yake ilikuwa imemwokoa.

40 Mnaona neno hilo *kuokoka*? Lifuatilieni hilo kote katika Biblia mwone kama si neno lile lile la Kiyunani kila wakati, *sozo*. Linamaanisha, "kuokoka kimwili," ama "kuokoka kiroho," mojawapo, linatumika. Linatafsiriwa vivyo hivyo mara zote mbili katika Kiyunani, *sozo*. "Imani yako imekuokoa." Imekuokoa na kitu gani? Dhambi. Imekuokoa na kitu gani? Suala la damu. "Imani yako imekuokoa." Na yote yamewekewa msingi juu ya imani.

41 Sasa, tunaona ya kwamba wakati Yesu alipokuwa hapa na akaonyesha ya kwamba Yeye Mwenyewe alikuwa ni Masihi, kulikuwa na wengi wao ambao hawakuamini jambo hilo, nao walitaka kumhesabu kama mpiga ramli, Beelzebuli, ibilisi aliyekuwa akifanya kazi ya Mungu. Yeyote wenu anakumbuka hilo katika Biblia? Vema. Yesu alisema, "Ninawasamehe hilo, lakini Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, kunena dhidi Yake hakutasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao."

42 Naye aliahidi wakati wa Mataifa, mwishoni mwa wakati wa Mataifa, ingekuwa ni aina ile ile ya ishara ya Masihi wakati wa Kiyahudi ulipokuwa ukimalizika, wakati wa Samaria ulipokuwa ukimalizika; yale matabaka matatu ya watu, watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Na mwishoni mwa wakati wa Mataifa, kama hivyo ndivyo alivyojithibitisha Mwenyewe kuwa Masihi hadi mwisho wa Mata-. . . , uh, kumalizia kwa Wayahudi, na kumalizia kwa Wasamaria, ndipo Yeye hana budi kutenda vivyo hivyo kwa Mataifa. Kama tukipitia tu juu ya theolojia basi Yeye alijiwakilisha vibaya, kwa kujithibitisha Mwenyewe kuwa Masihi kwao jinsi alivyofanya, na kutuacha tusiwe na ishara iyo hiyo.

43 Lakini kama mtavumilia kwa makini sasa, sikilizeni, ninyi mlio kwenye viti hivi na machela, kama mtaangalia kwa makini sasa sasa, Yeye anaweza tu kujithibitisha Mwenyewe kwamba yu hai, bali kuhusu uponyaji wako, ni bidhaa iliyokamilika. Kama alikuwa amesimama hapa usiku wa leo amevaa suti hii aliyonipa, asingeweza kukuponya. Kama ukija na kumwomba sana, na kumsihi akuponye, Yeye hawezi kufanya yale ambayo tayari amefanya, amekuachia hilo juu ya msingi wa imani yako. Hawezi kukuokoa kinyume na njia yako mwenyewe, mapenzi yako mwenyewe, wewe ni mtu mwenye hiari ya kujichagulia, unaweza kuukataa, ama unaweza kuukubali.

44 Mnaelewa dhahiri sasa? Hawezi kukuponya kinyume na mapenzi yako, hawezi kukuokoa kinyume na mapenzi yako, bali Yeye anaweza kujitambulisha Mwenyewe katika ahadi Zake, ndipo unalikubali juu ya misingi hiyo. Ni wangapi wanaelewa hilo sasa?

Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu, basi, tunapoomba.

45 Baba mwenye Rehema na Mtakatifu aliyemfufua Bwana wetu aliyebarikiwa kutoka kwa wafu, na amemkabidhi kwetu kama Kuhani Mkuu, akiishi daima kufanya maombezi tunapokiri yale aliyotufanyia, ameketi usiku wa leo kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, mkono wa kuume wa Ukuu, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Tunaukaribia utakatifu Wako usiku wa leo, Bwana, na kiti Chako cha neema kupitia Jina Lake litoshelezalo kwa yote alilotupatia, "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya."

46 Sasa, Baba wa Mbinguni, kunao wengi wamekuwa wakingojea juma hili, wameketi humu jengoni wakitarajia, wakiungojea usiku huu uje. Wanasema kwamba mamia wamekosa nafasi jengoni. Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe dhahiri sana kwa watu hawa, hata hakutakuwa na mtu mmoja mnyonge miongoni mwetu.

47 Ee Roho Mtakatifu Mkuu, tunapoiona saa tunayoishi, vivuli vinaanguka, mwisho umekaribia, na, Mungu, ninaomba ya kwamba utamjalia atahiri kila moyo, aondolee mbali kila kutokuamini na kila kivuli cha shaka. Nasi tunaomba ya kwamba atajidhihirisha Mwenyewe waziwazi sana miongoni mwetu usiku wa leo, hata hakutakuwako na mtu mmoja, kijana au mzee, ila atakayeona kwamba Yeye yupo hapa. Na jalia wamkumbatie kama Mwokozi wao na kama Mponyaji wao.

48 Jalia wasiookoka waokolewe, nao wagonjwa na waponywe. Na wale walioketi katika maeneo ya vivuli vya mauti, Nuru kuu na iwazukie, jalia wasimame waende nyumbani wakapate afya, ili utukufu wa Mungu uweze kujulikana kwenye Pwani ya Magharibi, ipate kusemwa kwa watoto wao, na wapendwa wao, na wale walio karibu, ya kwamba Yesu angali hai.

49 Sasa, Baba, tunafundishwa katika Biblia ya kwamba siku moja, siku moja baada ya ufufuo, ama siku ile ile, kwamba kulikuwa na mmoja wa wanafunzi Wake jina lake Kleopa, naye pamoja na rafiki yake walikuwa wakienda kwenye mji uitwao Emau, wameudhika, nao walikuwa wakirudi. Kuna wengi usiku wa leo katika hali hiyo, wanaofikiri ya kwamba kanisa limeshindwa, na kweli limeshindwa, bali Wewe hujashindwa.

50 Ndipo barabarani akaja Mtu kutoka kando ya barabara, na kuanza kuzungumza nao na kuwaelezea Maandiko, wakati alipowauliza huzuni yao na kushindwa kwao. Alifanya kana kwamba angepita, bali wakamshawishi aingie. Alipowaingiza ndani na kufunga mlango, ndipo akafanya jambo fulani kama vile tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, na mara wakajua ilikuwa ni Yeye. Akatoweka machoni pao kwa mlango wa nyuma, mahali fulani.

51 Wakiwa wachangamfu na wenye miguu myepesi wakaenda mbio, wakarudi Yerusalemu, wakiwaambia watu ya kwamba kweli Yesu alikuwa angali hai. Wakasemezana na kusema, "Je,

mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?"

52 Baba, ninaomba ya kwamba utamjalia atoke kwenye marefu haya usiku wa leo, aingie katika kila moyo, akizungumza nasi katika dakika chache zijazo, kisha ajionyeshe Mwenyewe. Jalia asimame kwenye jukwaa hili miongoni mwetu usiku wa leo, na kujionyesha Mwenyewe ya kwamba Yeye ni Yesu yule yule. Basi jalia wagonjwa wakimbie nyumbani upesi, wakisema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, Neno lilipotoka? Ilikuwa ni ajabu, lakini *Kitu fulani* kilikuwa kikizungumza nami wakati wote." Tujalie, Baba, nasi tutakusifu Wewe kwa ajili ya hilo maadamu tungali hai, na kulikumbuka sikuzote, kwa sababu tunaomba kwa uaminifu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

53 Sasa, kwa dakika chache tu, ningetaka tu kuwakumbusha Mathayo Mtakatifu 14:27:

> *Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni* moyo*; ni mimi; msiogope.*

54 Hapana shaka ilikuwa wakati jua lilipokuwa likitua, ilikuwa ni siku ya kutisha sana, kulikuwako na maelfu ya watu waliokuwa wamekusanyika kote, lakini yule mvuvi mkubwa mwenye mgongo mkubwa, mgumu na misuli alikuwa akisukuma hiyo mashua ndogo kutoka kwenye hizo kingo za mchanga wa ziwani. Walikuwa wakivuka, wakiagizwa na Bwana wao, wavuke ng'ambo ya pili, huku Yeye akiwaaga watu.

55 Na huku Simoni, labda ndiye mkubwa kuliko wote miongoni mwao, anausukuma maskini mtumbwi huo mdogo ufukoni, akapanda juu miongoni mwa hao mitume wengine, akaketi yapata katikati ya hicho chombo, akashika kasia lake mkononi mwake, basi wakati wao, labda, walivuta mara mbili au tatu, kisha wakawapungia mkono kusanyiko walilokuwa wakiliacha ukingoni.

56 Halafu wasema kwa sauti kuu, baadhi yao, "Rudini mkatuone tena, tungependa tuwe tukienda pamoja nanyi," kwa sababu walikuwa wameivutia mioyo yao, na waliwapenda watu hawa. Walikuwa wameuona mkono wa Mungu ukitenda kazi pamoja nao, nao walijua ya kwamba hawa walikuwa watumishi wa Mungu.

57 Jua lilikuwa linaingia wekundu lilipopita juu ya milima ya Galilaya, nayo mitaa ilikuwa imetulia, nayo anga ilikuwa imeanza kuingia giza wakati, nadhani, makasia yalipoachiliwa kidogo tu. Nami ninaamini hapana shaka ilikuwa ni yule kijana Yohana, alikuwa ndiye mdogo kuliko wote miongoni mwao, labda mtu aliye kwenye miaka yake ya thelathini, ndipo waliposimama kupumzika kidogo tu kwa sababu hicho chombo kilitengenezwa kwa mbao nzito, na makasia makubwa mno, nacho kilikuwa kizito, na mtu mmoja kwenye kasia kubwa na ilikuwa vigumu, labda wakati wa utulivu wa jioni, pepo zilikuwa

zimetulia na hapakuwapo na mawimbi ziwani, nao walikuwa wamevuta kwa nguvu sana, hapana shaka Yohana alivuta kasia ndani, na kusema, “Ndugu,” hebu na tuyaingilie mazungumzo yao, huenda alisema kitu kama hiki, “tunaweza kuwa na hakika ya kwamba hatumfuati mdanganyifu wa namna fulani.

58 “Mnajua, nakumbuka nilipokuwa mvulana mdogo,” huenda alisema, “Ninamkumbuka mama yangu akichukua magombo ya Biblia, naye alizoea kuketi na kunisimulia hadithi za watu wetu walipokuja kwenye nchi hii ambayo Mungu aliwapa, na ni wakati mzuri jinsi gani waliokuwa nao wakija, jinsi walivyotoka Misri, naye Yehova akawalisha huko nyikani kwa muda wa miaka arobaini. Nami nilizoea kusema, ‘Mama, walipataje chakula chochote nyikani?’

“Nami ninakumbuka maskini mama yangu mrembo, Myahudi alizoea kusema, ‘Yohana, kipenzi changu, Mungu alinyesha chakula chao kutoka Mbinguni kila usiku.’

“Nami ningemwambia hivi: ‘Mama, Mungu alipata wapi matanuri makubwa namna hii ya kuoka mkate?’

“‘Vema, unaona, Mpenzi, Mungu ni Muumba, si lazima Yeye awe na matanuri, Yeye hunena tu na anaumba, Neno Lake huumba.’

59 “Ndugu, leo hii niliposimama juu ya ule mwamba nyuma Yake, na kumwona akichukua hizo biskuti tano ndogo na samaki wawili, na kuumega mkate huo na kuwalisha watu elfu tano, nilijua Yeye alikuwa na uhusiano fulani na huyo Yehova Ambaye angeweza kuumba. Mnaona, ndugu, kama Yeye ni Yule tunayeamini kuwa Ndiye, nasi tunajua Ndiye, Mwana wa Mungu, basi kazi Zake zitakuwa kama Mungu, kwa maana Yeye alisema, ‘Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi.’

60 “Kwa hiyo hilo lilitosha kabisa kwangu, kwa kuwa ninajua ya kwamba Biblia ilisema ya kwamba hivyo ndivyo Yehova alivyoumba mkate. Basi ndugu, Yeye hakuupika, hakuuoka, Hakwenda baharini kuvua samaki, wala hakuwapika hao samaki, alivunja tu kipande cha samaki aliyepikwa, halafu aliponyosha mkono, kulikuwa na kipande kingine cha samaki tayari kimepikwa.”

61 Ninataka kuliuliza kusanyiko hili jambo fulani: Yeye aliachilia atomi ya aina gani pale?

62 “Kamwe hakulima ngano na kutengeneza mkate, alichukua tu hiyo biskuti, ama, huo mkate mdogo ambao aliupasua vipande viwili, na kumpa Simoni, ndipo alipoangalia nyuma kummegea Andrea kipande, kingine kilikuwa kimekulia juu yake. Nilimwangalia akifanya hivyo mara elfu tano au zaidi. Kwangu mimi, Yeye ni Yehova, Yeye ni Muumba.

63 "Laiti mama yangu angaliishi kuona hilo, ama, kuwa hapa leo kuangalia jambo hilo. Jinsi ningelitaka kwenda na kumshika, nimkumbatie, kasema, 'Mama, huyo ni Yehova yule uliyenena habari zake, kwa kuwa Yeye ni Muumba. Watoto wake walikuwa na njaa, kama tu walivyokuwa na njaa nyikani, Naye akaleta mkate kutoka mbinguni, na kuwalisha watu milioni mbili na nusu, na yu hapa leo, amesimama duniani, akiishi katika umbo la Mwanawe Mwenyewe, Bwana Yesu Mwokozi wetu, nilimwona, kwa nguvu za Baba Yake, akiumega huo mkate, na kuwagawia, nguvu zile zile za uumbaji, kwa hiyo ninajua kwamba Yeye kweli ni Mwana wa Mungu. Ninaamini hilo.'"

64 Simoni, akiketi moja kwa moja upande wa pili wa chombo, akipangusa jasho kutoka pajani mwa uso wake, akasema, "Ndugu, ningetaka kutoa ushuhuda wangu." Mwajua, kuna jambo fulani kulihusu wakati Wakristo wanapokusanyika pamoja na kuanza kushuhudia, kamwe hakuna mwisho wake, wanaendelea tu. Mtu hana budi kuwa na jambo la kusema, kwa sababu Yeye ni mwema sana kwetu hata tunataka tu kulielezea kwa njia fulani, wala kamwe hatupati mahali pa kusimamia, Yeye ni mwema sana.

65 Simoni, yule mvuvi mashuhuri, mwenye misuli migumu, ninaweza kumwazia akitoa ushuhuda wake, akasema, "Loo, ndugu yangu Andrea, aliyeketi papa *hapa* mbele yangu, ninakumbuka akiniambia ya kwamba alikuwa amekutana na Nabii wa namna fulani, ndipo akaja akanichukua twende mkutanoni siku moja. Nami nikakumbuka yale baba yangu aliyoniambia. Nanyi ndugu mnajua ya kwamba baba yangu alikuwa ni Mfarisayo. Nami nikakaa na dhehebu letu, ninii yetu...maana nilikuwa Mfarisayo, pia, yeye alikuwa ni Mfarisayo."

66 Naye akasema, "Mnajua kilichotukia? Ninakumbuka nikimsikia baba yangu, kabla hajaaga dunia, wakati alipokuwa anazeeka, nywele zake zilikuwa na mvi, siku moja aliniketisha chini kando ya meli, naye akasema, 'Simoni, maskini mwanangu, Baba daima ameamini ya kwamba ningeishi nipate kuiona siku ya kumwona Masihi. Ila sijui kama nitaishi sasa au la, huenda nikaitwa wakati wowote kujibu. Lakini Simoni, baba yangu alinipa habari hizi, nami ninakupitishia hizo.

67 "'Sasa, katika siku ya Masihi wa kweli, kutakuwako na mambo mengi sana yatakayoinuka, Simoni, ambayo ni ya uongo.'" Nasi tunajua Biblia ilisema lilitukia, daima linatukia. "'Lakini Simoni, usidanganyike, Mwanangu, kama yakija katika siku zako. Sasa, Simoni, itakubidi kudumu moja kwa moja na Maandiko upate kumjua Yeye, usichukue yale mtu mwingine asemayo juu yake, dumu na Maandiko, Simoni.

68 "'Sasa, Biblia inasema nabii wetu, Musa, alitwambia ya kwamba Bwana Mungu wetu anapaswa kutuondokeshea Nabii

kama yeye. Sasa, Simoni, Masihi huyu atakuwa ni Nabii, na i—ishara atakayotoa ya kwamba Yeye ni Nabii, kwamba Yeye—kwamba Yeye ni Masihi, itakuwa ni ishara ya nabii.

69 "'Na Simoni, unajua ya kwamba sikuzote tunawaamini manabii wetu, maana wakati manabii wetu wanaponena na yale anayosema yanatimia, basi Mungu alitwambia tumsikie nabii huyo, "Niko pamoja naye. Lakini kama akinena, wala yasitimie, basi msimwogope nabii huyo. Lakini yakitimia. . . " Sasa, imekuwa ni miaka mia nne, Simoni, tangu nabii wetu wa mwisho, tunajua ya kwamba nabii atakayeinuka atakuwa ni Masihi, nawe mtarajie, Yeye atafanya ishara ya nabii.'

70 "Basi niliposhuka siku moja ziwani, baada ya kuvuta juya usiku kucha na kuvunjika moyo, Andrea aliniambia, ndugu yangu, aliyeketi mbele yangu hapa, ya kwamba Yeye atakuwa mahali fulani. Nasi tulikuwa tukiingiza mashua zetu, nikawaona wanawake wote na wanaume wamekusanyika kutoka kwenye vibanda vidogo kando ya ziwa, nilishangaa yote hayo yalihusu nini, naye Andrea akasema, 'Simoni, huna budi kuambatana nami leo, kwa kuwa Masihi atazungumza leo, hapa chini.'

71 "Vema," akasema, "sasa, sikuamini ya kwamba huyo angeweza kuwa ni Masihi yeyote, bali ninakumbuka yale Baba aliyoniambia. Ndipo nilipoenda Mbele Zake, nilipomsikia akinena, kabla sijafika pale, kulikuwa na kitu tofauti kumhusu, alionekana kuwa ni Mtu aliyejua kile alichokuwa akizungumzia. Hakuwa akinena kama mwandishi, alikuwa akinena kama mtu aliyejua alichokuwa akizungumzia.

72 "Ndipo akageuza kichwa Chake kuniona nikija, na mara aliponiona, aliniangalia usoni, na kusema, 'Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona.'

73 "Ndugu, hilo lilitosha kabisa kwangu mimi. Si kwamba tu Yeye alinijua, alimjua maskini yule baba yangu mtauwa aliyeniambia niitazamie ishara hii, kwa hiyo nilijua huyo alikuwa ni Masihi, kwa sababu ilikuwa ndiyo ile ishara ambayo baba alisema Biblia ilisema itamfuata na kumfanya Yeye kuwa Masihi, kwa hiyo nilijua Yeye alikuwa Masihi."

74 Hapana shaka ilikuwa, basi, Filipo, akiketi nyuma kwenye shetri ya mashua, aligeuka, akamkumbatia Nathanaeli, na kusema, "Nathanaeli, nishuhudie, au utashuhudia?"

Loo, Nathanaeli, akiwa daima muungwana, alisema, "Endelea ukashuhudie hilo, Filipo."

"Vema," akasema, "nilipoona hilo likitendeka kwa Simoni, nilikuwa na hakika kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi, kwa sababu alikuwa akionyesha ishara ya Masihi.

75 "Kwa hiyo basi, nilijua ya kwamba rafiki yangu mwema hapa, Filipo alikuwa, ama, Nathanaeli alikuwa ni msomi mashuhuri wa Biblia, naye alikuwa ameisoma Biblia, alijua

kile Masihi angekuwa, kwa hiyo nikauzunguka mlima, maili kumi na tano, mpaka nikafika nyumbani kwa Filipo na, ama, nyumba ya Nathanaeli, hasa, nami nikabisha mlango. Mke wake akaniambia ya kwamba alikuwa nyuma bustanini. Nikaenda huko nyuma, nikamkuta amepiga magoti, akiomba, 'Ee Mungu wa Israeli,' hapo ndipo jambo fulani linapotukia, unapoanza kuomba, 'tutumie ukombozi!'

76 "Nami nikasimama nyuma, na moyoni mwangu, nikamshukuru Mungu kwamba nilikuwa na ujumbe kwa ajili yake, kwamba Mungu alikuwa amenitumia kuja mlimani kwa rafiki yangu. Ndipo alipoinuka na kukung'uta vumbi nguoni mwake, nikasema, 'Nathanaeli!'

"Naye akasema 'Filipo, nina furaha kukuona,' yeye . . .

"Upesi nikamwambia, 'Njoo, umwone Mtu tuliyemwona.'"

77 Kuna jambo fulani kulihusu, wakati wowote unapokutana na Masihi halisi, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, huwezi kutulia, inakubidi kumwambia mtu fulani, inaenea tu, inauchangamsha moyo wako, kamwe huwezi kuwa vivyo hivyo.

"'Njoo, umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, Yeye ni Masihi, mwana wa Yusufu.'

78 "Nanyi mwajua, Nathanaeli, akiwa ni msomi sana, pia alikuwa ni Farisayo kwelikweli, mpaka akasema, 'Sasa ngoja kidogo, sasa ngoja kidogo! Sasa, Filipo, hakika hujaenda kombo kwa mazingaombwe, ama kurukwa na akili. Sasa, unajua, kama Masihi angekuja, Yeye angeshukia kwenye dhehebu letu, angejitambulisha Mwenyewe kwetu, angeenda kwa Kayafa, kuhani mkuu. Kamwe asingezaliwa Nazareti, Kamwe asingeshughulika na kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha, ama kadhalika, huko chini. Unajua, kama alikuwa akija, angekuja kanisani *mwetu*, maana sisi ndio Mafarisayo.'"

79 Lakini, mwajua, msimamo huo haujawahi kuwaacha watu. Wala Mungu kamwe hajabadilika, Yeye hufanya yale anayotaka kufanya, Yeye hufanya yale aliyosema angefanya, Yeye huja, si lazima aje kwenye dhehebu lolote, Yeye huja tu kwa watu.

Kwa hiyo, tunaona, yeye alisema, "'Vema, sasa, njoo uone.'

"Akasema, 'Sasa, sasa angalia hapa, Filipo, ninaamini wewe ni msomi mzuri, wala sioni jinsi ungendanganyika na kitu kama hicho.'

"Nami nikamwambia, 'Nataka kukuuliza jambo fulani: Hivi huyajui Maandiko Matakatifu?'

"'Naam, nimeyasoma tangu utotoni.'

"'Vema, niambie basi, niambie basi kama unayajua Maandiko, Masihi atakuwa namna gani wakati atakapokuja?'

"'Mbona, Yeye atazaliwa na bikira.'

80 "'Na, ataishi maisha ya namna gani? Yeye atatupa ishara ya namna gani? Mnajua, sisi ni Wayahudi, tunatafuta ishara. Mungu alitwambia tumtazamie nabii, na tuone yale aliyosema, kama yakitimia, yeye alikuwa ni nabii wa Mungu. Masihi atakuwa ni ishara ya namna gani?'

"'Vema, kulingana na Maandiko, Yeye atakuwa ni Nabii.'

"'Sasa, ninataka kukuuliza jambo fulani: Unamkumbuka yule mvuvi mzee ambaye ulimnunua yule samaki kutoka kwake siku ile, naye asingeweza kukutilia sahihi risiti?'

"'Naam.'

"'Loo, jina lake lilikuwa Simoni.'

"'Naam, nilikuwa ninamjua maskini baba yake hapa juu kwenye si—sinagogi.'

81 "'Vema, mara alipokuja Mbele ya huyu Yesu wa Nazareti, alimwangalia moja kwa moja usoni na kumwambia jina lake lilikuwa ni nani, na kumwambia yeye alikuwa ni mwana wa nani. Mbona, haitanishangaza, Nathanaeli, utakapoenda mbele Zake, kama Yeye hatakwambia wewe ni nani.'

"'Loo,' akasema, 'sasa laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?'"

Vema, nafikiri alimpa jibu zuri, jibu ambalo linapaswa kumridhisha kila mtu, akasema, "Njoo, uone."

82 Usiketi nyumbani na kulikosoa, njoo, uone. Njoo, ujionee mwenyewe, unapaswa kuhusika kiasi hicho. Njoo, uone, lichunguze kwa Maandiko, uone litakavyokuwa.

83 Basi walipokuwa wakienda mlimani wakizungumza, mara wakafika mahali ambapo Yesu alikuwa akiwaombea wagonjwa. Labda alikuwa kwenye mstari wa maombi, ama labda alikuwa tu amesimama kwenye kusanyiko, lakini mara alipokuja Yesu aliangalia huko na kumwona. Mwajua, kuna kitu fulani kuhusu Maandiko hayo, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Alivutia usikivu wake, Naye akasema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

84 Nilisema hivyo wakati mmoja, ndipo mtu fulani akasema, "Hakika, alikuwa amevalia kama Mwisraeli." La, wote walivalia vivyo hivyo, Waarabu, Wayahudi, Wayunani, wote walivalia sawa, vazi la kimashariki.

Kasema, "Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!" Hilo lilimtoa nguvu.

85 Angalia kile Nathanaeli alichosema, "Rabi," ambalo linamaanisha *mwalimu*, *bwana*, "Rabi, hii ndiyo mara ya kwanza uliyopata kuniona, hii ndiyo mara ya kwanza niliyopata kukuona Wewe. Ulipataje kunijua?"

Yesu akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Hilo lilitosha.

Kasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli."

86 Kama huyo alikuwa ni Yesu jana, na Yeye ni yule yule leo, huyo ni Yesu leo. Mnaamini hilo? Hakika.

87 Sasa, tungeweza kuendelea tu mbele zaidi na zaidi katika Maandiko, lakini ninajaribu kuushikilia wakati wangu kusudi msichoke, na wengi. . . Ninataka kugusia Andiko moja zaidi, ikiwezekana, kabla hatujafika kwenye mstari wa maombi, hebu na tuchukue tu jambo moja zaidi.

88 Baada ya Filipo kumaliza kushuhudia, Andrea, labda walianza kuuendesha huo mtumbwi, akasema, "Hebu kidogo, ndugu, hebu nishuhudie." Mnajua, kuna kitu kama hicho, daima unataka kushuhudia wakati kweli umekutana na Yesu. Akasema, "Hebu nishuhudie kwa ajili yetu sote, ili kwamba sote tutajua." Kasema, "Mnakumbuka wakati ule ambao Yeye alitwambia asubuhi ile, ama, siku iliyotangulia, 'Kesho tunashuka kwenda Yeriko'?"

89 Na sasa kutoka Yerusalemu hadi Yeriko ni moja kwa moja chini ya mlima, unapanda moja kwa moja na kushuka mara moja hadi Yeriko. "Lakini alikuwa na haja ya kupitia Samaria. Nasi mara nyingi tulishangaa, kwa nini alitaka kwenda mpaka Samaria kabla hajashuka kwenda Yeriko? Naye akasema alikuwa na haja ya kwenda." Kwa nini? Baba alikuwa anamtuma.

90 "Nanyi mnakumbuka, tulifika kule yapata adhuhuri, Naye alikuwa amechoka sana, nasi tulifadhaika kwa sababu Yake. Naye akaketi kando ya kile kisima kidogo cha umma karibu, mandhari ndogo pale pamoja na. . . " Kasema, "Aliketi chini pale kupata. . . Tulidhani angekunywa maji, wala hapakuwapo, hamna kitu pale cha kunywea, kwa hiyo sisi, Yeye akatutuma mjini kununua vyakula, chakula.

91 "Nanyi mnakumbuka? Loo, wao. . . Tulipomaliza na kuanza kurudi, tulipokuwa tukipanda ilitokea tulisikia kitu fulani kisimani, ndipo tukajificha nyuma ya vichaka, halafu tukachungulia kuona ilikuwa ni nini. Basi huyo hapo mwanamke mwenye sifa mbaya akija kisimani, nasi tukatega masikio.

92 "Sasa, nitanukuu, ndugu, nanyi nyote mtakumbuka hili," ninaweza kumsikia Andrea akisema. "Mnakumbuka, mwanamke huyo alishusha winchi achote maji? Ndipo alipoyapandisha maji, tulisikia, tukachungulia kule, tuone kile atakachosema kuhusu mwanamke huyu, mwenye sifa mbaya. Alikuwa nje ya makanisa, alikuwa ni asiyehusika."

Jambo lingine, yeye alikuwa ni Msamaria. Ubaguzi mkubwa, Wasamaria na Wayahudi hawakuchangamana.

93 “Nasi tulimwona mwanamke huyu, mwanamke mrembo, bali tulijua alikuwa na sifa mbaya, jinsi alivyokuwa amevalia. Nao wakapandisha maji, nasi tukamsikia akisema, ‘Nipe maji ninywe, ewe mwanamke. Nipe maji ninywe.’

94 “Nanyi mnakumbuka jinsi tulivyoshangaa kwamba Bwana wetu angekuwa na uhusiano wa namna yoyote na mwanamke kama *huyo*? Na kwa hiyo, mwanamke huyo akasema, ‘Bwana, si kawaida Kwako kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, msaada wowote kwa sababu Wewe ni Myahudi.’

95 “Basi mnakumbuka yale aliyosema? ‘Laiti ungalijua ni Nani unayesema naye ungeniomba Mimi maji unywe, nami ningekupa maji ambayo haitakubidi kuja hapa kuyateka.’

96 “Naye akasema, ‘Kisima ni kirefu, wala huna kitu cha kuchotea.’ Nanyi mnakumbuka, ndugu, jinsi mazungumzo yalivyoendelea kuhusu Myahudi na Msamaria.”

97 Sasa, ninaamini, nitasema hivi, ninaamini ya kwamba Yesu alikuwa akijaribu kuwasiliana na roho yake, akizungumza naye. Baba alikuwa amemtuma huko juu. Hebu niondoe hilo niani mwenu, wekeni niani mwenu kila kitu ambacho nimesema sasa, ninataka kuondoa hili. Baba . . . Yeye alisema, “Sitendi neno mpaka Baba anionyeshe.”

98 Basi hapana shaka Baba alimtuma huko juu, na kusema, “Kwea hata utakapoona kisima hiki,” Yeye hakuwa amewahi kuwa kule hapo kabla, “uketi hapo chini, na kungojea. Ninakutuma Wewe kule, na hayo mengine yote yatashughulikiwa utakapofika huko.”

99 Vema, alimwona mwanamke huyu, na hapana shaka huyo alikuwa ndiye, kwa hiyo akaanza kuzungumza naye apate roho yake. Sasa, kumbukeni, Yesu angeweza kutambua mawazo na makusudi ya moyo. Na hivi Biblia yetu haitwambii, Waebrania, mlango wa 4, ya kwamba Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huchoma hata kugawanya na mafuta ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo na nia? Neno la Mungu!

100 Yesu alikuwa ndiye hilo Neno, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu.” Hilo hapo Neno la Mungu likipenya ndani ya nafsi ya mwanamke huyo, likitafuta mahali shida yake ilipokuwa. Ni wangapi katika darasa langu usiku wa leo wanaojua shida yake ilikuwa ni nini? Inua mkono wako. Hakika. Alikuwa na waume watano.

“Kwa hiyo Yeye akasema, ‘Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.’

“‘Mbona,’ akasema, ‘Sina mume.’

101 Naye Andrea akasema, “Ndugu, mnakumbuka tulichowazia? ‘Uh-loo, uh-loo, Yeye amekosea wakati huu.

Hakika amekosea hapo juu ya Msamaria huyu, huenda ikafanya kazi kwa Wayahudi, bali sijui kuhusu Wasamaria. Hakika amekosea sasa, maana yeye anasema mwenyewe hana mume yeyote.'"

102 Sasa, kama mtakumbuka tu, jambo lile lile lilimpata Myahudi, pia, wakati mmoja, wakati Malaika wa Mungu aliposhuka katika mwili wa kibinadamu huko Sodoma na Gomora, kulikuwa na mmoja wa malkia wa wanawake wa Kiyahudi, Sara.

103 Billy Graham na Oral Roberts wa kisasa wanashuka katika mji wa Sodoma na kuhubiri Injili, lakini kulikuwa na Mmoja wao aliyebaki nyuma, akizungumza na Kanisa teule. Kamwe hakushuka kwenda kwenye kanisa huko Sodoma, alikuja kwa walioitwa watoke, Kanisa teule, Ibrahimu. Ndiyo kwanza tuyapitie.

104 Basi alipokuwa akizungumza na Ibrahimu, sasa, Yeye alikuwa mgeni, Naye akasema, "Ibrahimu," na kumbukeni, kamwe hakumwita *Abramu*, siku chache tu hapo kabla jina lake lilikuwa limebadilishwa kutoka *Abramu* likawa *Ibrahimu*, kasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara?" Sio *Sarai*, *Sara*, jina lake la kifalme, ndiyo kwanza apewe hilo siku chache hapo kabla. "Yu wapi Sara, mkeo?"

Alijuaje alikuwa ameoa? Pia alijuaje alikuwa na mke? Na alijuaje jina lake lilikuwa Sara?

Ndipo Ibrahimu akasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

105 Akasema, "Nitakuzuru, nitalitimiza, umengojea miaka ishirini na mitano kwa ajili ya mtoto huyu mchanga, katika muhula wake wa maisha nitakuzuru."

106 Ndipo Sara, akiwa hemani nyuma Yake, akacheka moyoni mwake, akawaza moyoni mwake, "Mimi, mwanamke mkongwe, mwenye umri wa karibu miaka mia moja, ati nipate raha na bwana wangu tena, mume wangu? Mimi, mwanamke mkongwe mwenye umri wa miaka mia moja, naye karibu umri wa miaka mia moja, niweze kuwa na raha tena pamoja naye? Hilo haliwezekani kabisa."

107 Naye huyo Malaika, yule Mtu aliyekuwa mwanadamu, akila nyama, akinywa maziwa na kula ugali, naye Ibrahimu akasema ilikuwa ni Mungu, akasema, "Kwa nini Sara akacheka hemani, akisema moyoni mwake 'Jambo hili litawezekanaje?'" Alitilia shaka.

108 Sasa kumbukeni, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu," ya kwamba Roho yuyo huyo aliyewakilishwa katika mwili wa mwanadamu, ambaye Ibrahimu alimwita Elohimu. . . Kuna mtu anayejua maana ya *Elohimu*? Hakika, "Mwenyezi, Ajitoshelezaye kwa Yote."

109 Ibrahimu, yule mzee wetu, alimwita *Elohimu*. Alijiwakilisha Mwenyewe katika mwili wa nyama, akila na kunywa, na kama tu mwanadamu mwingine yeyote. Naye alifanya ishara hiyo kwa Kanisa teule kabla hajaiangamiza Sodoma. Loo, msilikose, ndugu, saa hiyo imewadia. Elohimu! Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Wakati mwili Wake umeketi mkono wa kuume kufanya maombezi kwa ajili ya Kanisa Lake, Roho yuyo huyo akiishi ndani ya watu Wake, Mungu, akidhihirishwa katika umbo la Roho Mtakatifu ndani ya watu Wake, akifanya jambo lile lile (Mnaliona?) kwa Mataifa.

110 Tumekuwa na miaka elfu mbili tangu tuwe nayo, bali Yeye alisema itakuwa wakati wa jioni. Nabii alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni. Kutakuwako na siku ambayo haitaitwa usiku wala mchana."

111 Sasa, j-u-a huchomoza mashariki na kutua magharibi, naye M-w-a-n-a, kama vile j-u-a la Mungu, huyu ni M-w-a-n-a wa Mungu, Yeye alikuja kwanza mashariki. Tumekuwa na siku yenye utusitusi, tumekuwa na ya kutosha kujiunga na kanisa, na kuunda dhehebu, na kuwaingiza baadhi ya watu, kuandika majina yenu kwenye vitabu, na kupata msamaha wa dhambi yenu, lakini nabii alisema, "Wakati wa jioni itakuwa Nuru." Ni kile . . .

112 Tuko papa hapa kwenye Pwani ya Magharibi, tuko chini ya nusu maili kutoka baharini, kama tukivuka, tumerudi mashariki tena. Hiyo ndiyo sababu dhambi inazidi, mawimbi yameieneza kote, nayo imechafuka kabisa. Lakini Yeye alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni."

113 Sasa, Yeye alikuwa akimshughulikia yule mwanamke Msamaria, nao hao ndugu chomboni wakasema, "Mnajua nini? Sote tulifikiri kwamba alikuwa amenaswa katika mtego. Tunashangaa atafanya nini sasa, yeye alikana, akasema, 'Sina mume.'"

114 "Bali sikilizeni yale Yeye aliyosema." Ninaweza kumsikia Andrea akisema, "Lakini ndugu, mnakumbuka aliyosema? Alisema, 'Umesema kweli. Umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Umesema vema.'

115 "Sasa, tulimdhania mwanamke huyu Msamaria, kwa kuwa ni mwovu, kwamba angesema, kama wahubiri waliofunzwa vizuri walivyosema, aseme, 'Vema, hapana shaka wewe ni Beelzebuli.'" Alijua zaidi kumhusu Mungu kuliko wahudumu wengi wanavyomjua siku hizi. "Yeye alisema, 'Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.'" Sasa, yasikilizeni maneno yake, yasomeni, Yohana Mtakatifu 4, "'Naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Sisi,'" sisi, Wasamaria, "'tunajua Masihi yuaja, naye Masihi atatuambia mambo haya, hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi. Lakini u Nani Wewe?'

"Yeye alisema, 'Mimi ninayesema nawe Ndiye.'

116 "Ndipo akakimbia mjini, na kusema, 'Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Si hiyo ndiyo ishara ambayo Masihi alipaswa kuonyesha?'"

117 Nayo Biblia ilisema, "Watu wa Samaria walimwamini kwa sababu ya yale yule mwanamke aliyowaambia Yeye amefanya." Je, huyo alikuwa ni Yesu jana? Huyo angekuwa ni Yesu leo, endapo Yeye ni Masihi yeye yule. Mengi zaidi tungeweza kuyaendea, hatuna muda.

118 Yapata wakati huo, wakayarudisha makasia majini, wakavuta mara chache. Mnajua, wakati wote walipokuwa wakishuhudia, walikuwa watulivu sana, lakini mnamo wakati walipoacha kushuhudia, kama wakati ambao kanisa linapoacha kushuhudia, kumpa Mungu sifa na utukufu, hapana shaka Shetani aliangalia juu ya kilima, akasema, "Loo, hilo... Nimewapata mahali hasa ninapowataka, wameondoka bila Yeye."

119 Ninahofia hivyo ndivyo kanisa limefanya leo. Mlivutiwa sana katika kama wewe ni mfuasi wa Foursquare, ama Assemblies, ama Umoja, au Uwili, ama lolote lile, mumevutiwa sana kwamba hamtajenga jengo kubwa kidogo kuliko hilo lingine, ama hamtafanya kitu kikubwa zaidi, ama kuwa na Kadilaki kubwa zaidi, ama kitu bora kuliko hao wengine, nafikiri kwenye mipango yetu mikubwa na mashirika yetu tumeondoka bila Yeye.

120 Shetani aliona jambo hilo naye akaanza kupuliza kwa pumzi yake ya sumu, akiyarusha maji juu, kasema, "Nitawazamisha."

121 Loo, naam, anapulizia kanisa la Kipentekoste pumzi yake ya sumu moja kwa moja. Ninajua Wapentekoste wengi tayari wameachana na mawazo ya uponyaji wa Kiungu. Hakika, hawaamini jambo hilo. Nilienda kwenye kanisa la Kipentekoste si muda mrefu uliopita kuchukua viti, tulikuwa na ghala ya silaha, na maelfu walikuwa wamesimama nje, nilishuka nikamwomba ndugu huyu Mpentekoste, alikuwa na viti kama mia tano, nikasema, "Ninaweza kuvikodi kutoka kwako, Ndugu?"

Akasema, "Kufanyia ibada hiyo ya uponyaji?"

Nikasema, "Naam, bwana."

122 Akasema, "Nisingemruhusu mtu kuketi kwenye viti vangu ambaye anaamini katika uponyaji wa Kiungu." Haya basi, hiyo ni Pentekoste. Msiwacheke Wabaptisti.

123 Pumzi yake ya sumu! Mlienda kombo kupita kiasi kwa mambo ya kimadhehebu, mkaenda kombo kwa mambo makubwa, mkijaribu kuiga Hollywood, mkijaribu kufanya mambo kama wanayofanya hapa kwenye Pwani ya Magharibi, ama kwenye pwani nyingine yoyote, mkijaribu kuuiga

ulimwengu, aliwaona bila Yeye, mkaangua lundo la shule mahali fulani, kundi la wahubiri wa kiangulio. Hiyo ni kweli.

124 Sikuzote nilimhurumia kuku wa kiangulio, ni ninii tu, "*Chwi*, *chwi*," wala hakuwa na mama yeyote. Hivyo ndivyo tunavyowatoa wahubiri siku hizi, kwa digrii za saikolojia. Shirika letu kuu, maarufu la Kipentekoste, sasa kabla mmishenari hajaweza kwenda ng'ambo, shirika kuu la Pentekoste, inawabidi kwenda mbele ya mwanasaikolojia kuona kama akili zao ni sawa.

125 Mmerudi nyuma mnapofikia hapo. Sawa. Akili yetu ni nani? Ni Roho Mtakatifu, Yesu. Lakini tunalo hilo, tunawapeleka mbele ya madaktari, wanasaikolojia, watu wa ulimwengu, kuona kama akili zao zina nguvu za kutosha kuwa mmishenari. Huh! Loo, jamani, pepo za sumu hakika zinavuma.

126 Imelifikisha kanisa mahali, huwezi kutofautisha Wapentekoste tena na mtu mwingine yeyote, wote karibu wanafanana. Wanazunguka-zunguka, wanawake wetu wamevaa maskini nguo za kipunguani, na nanii zetu, wengi wa ndugu zetu wanaenda huko nje nawe unawaona wamesimama barabarani wakifanya mizaha ambayo, *hmm*, mabaharia walevi wasingeweza kufanya. Unawaona huko chini, wake wawili ama watatu mbalimbali, wakiishi kanisani, na kuwafanya mashemasi, na chochote kile, na kutoka nje na kutenda kama tu walimwengu.

127 Husikii mikutano ya maombi ya mtindo wa kale tena, na kumlilia Mungu, yote yamesahaulika, yote yamepita, mnaona. Ninahofia tulienda bila Yeye. Hamwoni hivyo?

128 Tulikuwa na vita, na pesa nyingi zikaingia, nazo pesa zikaanza kutoka kila mahali, nami nafikiri tulifuatilia majengo makubwa, na madhehebu makubwa, na mambo makubwa, na tukamwacha Yeye. Hiyo ni kweli.

129 Ndipo ikafikia mahali ambapo matumaini yote yalikuwa yamekwisha, kilikuwa tu karibu kuzama, laiti ningalidumu katika jambo hili kwa muda kidogo, lakini niliahidi kutofanya hivyo, hayo mawimbi yakipiga kote, walikuwa karibu wamekwisha. Lakini mnajua, nina faraja hii ya kuwaambia: Yeye hakuwa ameenda mbali sana. Mnajua alilofanya? Alijua hilo lilikuwa linakuja kutimia, alijua walikuwa wanaenda kuingia katika hali hiyo, ndipo basi akajua mlikuwa mnaenda kuingia katika hali hiyo. Hakika. Alifanya nini? Ili aweze kuwaangalia, alipanda mlima mrefu kuliko yote nchini. Kadiri unavyopanda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Naye akapanda juu ya mlima, Naye alikuwa huko juu ya mlima akiwaangalia huko nje wakipiga makasia.

130 Laiti ningaliweza kuimba, "Jicho Lake liko kwenye shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia." Hivi hamjui hilo? Anaona taabu na shida zako, anaona jinsi ulivyo mgonjwa,

anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wako. Si kwamba tu alipanda mlima, bali alipanda Kalvari, kisha akapanda juu ya mwezi na nyota, mpaka akaketi kwenye kiti cha enzi cha Mungu, mpaka anaweza kuona ulimwengu. Anaangalia, anangojea.

131 Kwenye usiku wa manane tu, wakati matumaini yote yalikuwa yamekwisha, maskini huo mtumbwi ulirushwa-rushwa kama kifuniko cha chupa huko nje, wakati pepo elfu kumi wa baharini walipokuwa wameapa wangewazamisha hao wanafunzi usiku huo, maana walikuwa wameondoka bila Yeye (Hivyo ndivyo Shetani anavyosema leo, “Nimelipata kundi hilo la Kipentekoste, ninawayumbisha. Wanazozana, hakuna mapatano kwao, wao ni kama tu walimwengu. Ninawayumbisha huku na huku kwa nguvu niwezavyo, hivi karibuni nitawayumbisha wawe kundi baridi, la kawaida.”), lakini moja kwa moja katika saa hiyo kuu huyu hapa Yeye anakuja, akienda kwa miguu juu ya bahari.

132 Ndugu, dada, sikiliza katika kufunga, jambo lile lile linatukia sasa lililotukia wakati huo, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, na kuwarudisha kwenye usalama, walikiogopa, Kilionekana cha kutisha kwao, walidhani kilikuwa ni kivuli. Na siku hizi Kristo anapokuja akitembea kwetu kwa nguvu Zake za Kimasihi, pamoja na ishara Yake ya Kimasihi, kama tu alivyosema, tunasema, “Ni telepathia, ama pengine, labda, mpiga ramli. Labda ni *hiki*, *kile*, *kinginecho*.” Wala hawajui ya kwamba Maandiko yalitoa ahadi.

133 Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na kama angeweza kunena usiku wa leo, angeiambia mioyo yenu, kuwafariji ninyi hapa mlio wagonjwa, “Msiogope; Ni mimi; msiogope.” Hili *hapa* Neno Lake linalotoa ahadi, haya *hapa* aliyosema, aliyoahidi. Ninaamini ya kwamba Yeye yupo hapa sasa. Mnaamini vivyo hivyo pamoja nami?

134 Angalieni! Loo, enyi watu, nisikilizeni kwa dakika moja tu. Vipi kama angekuja akitembea miongoni mwetu usiku wa leo, naye angejithibitisha Mwenyewe ya kwamba Yeye ndiye Masihi? Je, ungeogopa kusema, “Bwana Yesu, ninakukubali Wewe kama Mponyaji wangu, siogopi, daktari alisema saa zangu zimekwisha, ni usiku wa manane, nina kansa; ni—nina ugonjwa wa moyo; ninakufa; mimi ni kiwete, wanasema kamwe sitatembea, bali sikuogopi Wewe”?

Ungemsikia akisema, “Usiogope, ni Mimi, niliahidi nitafanya jambo hili. Kama ilivyokuwa katika siku. . . ” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

135 . . .?. . .-ngeweza kusema maishani. Wewe ni Mungu wetu, nasi tunakupenda. Na Wewe milele hata milele, ni Mungu. Ninakuomba, Baba, ya kwamba utatusaidia usiku wa leo. Sasa, laiti ungaliingia tu miongoni mwetu usiku wa leo, Baba, baada

ya ujumbe huu mdogo uliokatwakatwa, kuwafanya watu waone kwa Biblia kile ulichokuwa, na zilizo ahadi Zako!

136 Ulijiwakilisha Mwenyewe, na kujithibitisha Mwenyewe, na hiyo ilikuwa ndiyo ishara kwamba Wewe uliwathibitishia ya kwamba ulikuwa Masihi kwa Msamaria na Myahudi pia, bali kamwe hukufanya hivyo mbele ya Mataifa, hata wakati mmoja. Lakini Wewe uliahidi ungefanya hivyo katika siku za mwisho, ninii tu, sio kama ilivyokuwa katika Nuhu, bali kama Sodoma kabla ya ule Moto, hapo ndipo ulipofanya jambo hilo, hapo ndipo ulipomfanyia Ibrahimu ile ishara, lile Kanisa lililoitwa litoke.

137 Ninaomba, sasa, Baba, ya kwamba ninaamini kwa moyo wangu wote ya kwamba watu, Kanisa Lako, limeitwa kutoka katika kila shirika, kila dhehebu, Methodisti, Baptisti, Katoliki, Presbiteri, lolote lile, wao ni Kanisa kwa sababu wamezaliwa katika Mwili wa kisiri wa Kristo. Wengi wao wamewakilishwa hapa usiku wa leo, Baba. Ninaomba ya kwamba utatujalia baraka tunazoomba.

138 Mimi sijitoshelezi, Bwana, hakuna lingine niwezalo kusema, ninaweza tu kulinukuu Neno Lako, kuwanukulia tu watu jinsi lilivyoandikwa, na kuwaambia. Sasa ni juu Yako kushuhudia kama nimesema kweli au la. Ninaomba ya kwamba utafanya hivyo, ili kwamba kila mtu hapa ndani aweze kukukumbatia Wewe na kusema, “Ingia kwenye maskini chombo changu, Bwana.”

139 Na mara alipoingia chomboni, Biblia ilisema, “Mara wakafika ufukoni.” Ee Mungu, haitachukua ila kidogo tu kuwapa afya, waponywe, ama waokoke, wakati watakapokualika, Nawe uingie ndani yao, katika ganda lao dogo, wakati wakisafiri kwenye barabara kuu ya maisha.

140 Wengi wako hapa, hapana shaka, usiku wa leo, Bwana, huku mawimbi ya maradhi yakiwashambulia, kansa, TB, ugonjwa wa moyo, wako karibu kuanguka, matumaini yote yamekwisha. Lakini jalia wasiogope usiku wa leo, Bwana, kwa kuwa tunaweza kusikia Sauti hiyo ya kufariji, kupitia Neno Lako ikisema, “Ni mimi; changamkeni; msiogope.” Tutakusikiliza sasa, Baba. Hili ni Neno Lako, uliliahidi.

141 Mimi, sisi ni watumishi Wako, siwezi kufanya hivi kwa upako ambao Wewe huenda ukanipa, itakubidi kuwatia mafuta, pia, kuamini jambo hilo, Baba, kwa maana ulipoenda katika nchi Yako Mwenyewe, matendo mengi makuu usingeweza kufanya kwa sababu ya kutokuamini kwao. Hapo ndipo Wewe uliposema nabii hakosi heshima ila katika—katika jamii yake mwenyewe, nchi ya—yake mwenyewe, ama, nchi. Nami naomba, Bwana, ya kwamba utaliheshimu Neno Lako usiku wa leo, na kulifanya liishi upya mbele ya watu hawa.

142 Baba, waangalie, wao ni wagonjwa, ni wahitaji, wamelala kwenye chumba hiki chenye joto, mamia yao walirudi, nao

wamesimama mpaka viungo vyao vinakakamaa na kuuma. Mungu, jalia Shetani aondoke mahali hapa sasa, jalia imani ya kweli ya Mungu ije ikiingia, jalia waelewe. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, tunapojikabidhi wenyewe na kusanyiko hili Kwako. Amina.

143 Sikilizeni tu wimbo huo, *Amini Tu.* Ninaweza kuwaona mitume. Siku kumi hapo kabla, walikuwa wamepewa uwezo wa kutoa pepo, kuponya wagonjwa, nao hawa hapa, wakiwa na mvulana mwenye kifafa, wameshindwa. Labda walikuwa wakipiga mayowe, na kukanyaga kwa kishindo, na kummwagia mafuta, na kupaza sauti, "Toka, ewe ibilisi!" Ibilisi huyo alikaa tu papo hapo. Kwa hiyo—kwa hiyo huyu hapa Mwana wa Adamu akishuka mlimani, Mwana wa Mungu, wakati Shetani alipojua hilo, alijua hakuwa akikutana na hao mitume.

144 Huyo baba akasema, "Bwana, mrehemu mwanangu, amepagawa sana na pepo. Mara nyingi, yeye huanguka motoni na ndani ya maji kumwangamiza. Nilimleta kwa wanafunzi Wako, wasingeweza kumponya."

145 Vema, kwa nini wasingeweza kumponya? Si kwa sababu hawakuwa na nguvu, kwa sababu hawakuamini. Hiyo ni kusema, usiku wa leo, ukitoka hapa ukiwa mgonjwa, si kwa sababu Mungu hana nguvu, Yeye amekupa; ni kwa sababu huliamini, hivyo tu. Jambo lile lile. Yesu alisema, "Ninaweza kama ukiamini." Hiyo ni kweli? Huna budi kuamini.

146 Billy, aligawa kadi za maombi? B, moja hadi mia moja. Kuna kadi za maombi B, moja hadi mia moja. Sasa, ni wangapi waliokuwa hapa wakati hao wavulana waliposambaza kadi? Hebu tuwaone. Sasa, mnajua walichofanya, wanazileta hizo kadi, wanazichanganya, ili mpate kadi, mtu yeyote anayeitaka. Huenda ukapata namba moja, huyo mwingine apate namba nane, na mwingine apate namba kumi na sita, mwingine apate thelathini na mbili, hujui itakakokuwa, kwa hiyo huyo mvulana hajui, hajui lolote kuhusu kadi za maombi. Ndipo anaposhuka, unasema, "Baba yako ataita kuanzia wapi, usiku wa leo?" Hajui, mimi sijui, lakini tunaita kutoka popote Roho Mtakatifu anapoweka juu yangu.

147 Nilikuwa nikiwaita watoto wadogo hapa, kasema, "Njoo huku, Kadogoo, na uhesabu, mahali utakaposimama, basi—basi tutaanzia hapo." Mama angemwambia Kadogoo mahali pa kusimamia, ili isingeninii, mnajua kamwe haifanyi kazi, kwa hiyo njia hii ina mamlaka.

148 Tulianzia wapi usiku uliopita, ndugu? Tulianzia moja, sivyo na tukapanda hadi, naam, tukapanda kufikia moja hadi kumi na tano. Hiyo. . .Tunataka tu kuchukua wachache. Mtu mmoja anapaswa kufanya hivyo, la sivyo hata si lazima uje huku hata kidogo, wewe amini tu. Kuna wengi zaidi wanaoponywa huko nje kuliko walio hapa juu, hata hivyo.

149 Hebu tuanzie mahali pengine usiku wa leo. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Hebu tuseme, hebu tuanzie wapi? Moja hadi mia moja. Tuanze tu kusudi tupate. . . Hebu tuanzie mahali pengine mbali na moja. Ulisambaza kutoka moja hadi mia moja katika B. Hiyo ni kadi ya maombi B, kadi ya maombi B. Hebu tuanze kutoka thelathini na tano. Hiyo ingekuwa thelathini na tano, arobaini, arobaini na tano, hamsini. Hao wangekuwa—hao wangekuwa kumi na watano hapo.

Kadi ya maombi B, thelathini na tano, ni nani aliye nayo? Una hakika? Um, samahani? Loo, hapa. Samahani. Njoo papa hapa, mama.

150 Sijui kama ninyi jamaa wadogo mngerudi nyuma moja kwa moja hivi, enyi watoto, tafadhalini, papa hapa, moja kwa moja huku nyuma madhabahuni, wapenzi, tafadhalini. Ninyi ni watoto wadogo wazuri sana, mmeketi hapo kimya sana nilipokuwa nikihubiri.

151 B. . . Hiyo namba niliyokuwa nikitaka kuita ilikuwa gani? Thelathini na tano. B, thelathini na tano. Vema. Ni nani aliye na thelathini na sita? Kadi ya maombi thelathini na sita, B, thelathini na sita. Vema, mama. Thelathini na saba. Ni nani aliye na thelathini na saba? Vema, mama. Thelathini na nane, thelathini na nane. Ni nani aliye na thelathini na nane? Yeyote-. . . ? Thelathini na nane, thelathini na tisa. Ni nani aliye na kadi ya maombi B, thelathini na tisa? Vema. Arobaini. Vema. Arobaini na moja, arobaini na mbili. Arobaini na mbili, sikuiona.

152 Sasa, labda mtu fulani ni kiziwi usiku wa leo, ambaye hatasikia. Angalia kote kwenye kadi ya jirani yako. Unaona? Huenda ikawa mtu fulani hawezi kusimama. Sasa, hilo halimaanishi wataponywa. Hiyo ni—hiyo ni. . . Inahitaji imani yako katika Mungu, nimewaambia hilo, imani yako katika Mungu.

153 Arobaini-. . . Hebu tuone, nilianza na gani tena? Thelathini na sita, thelathini-. . . ? Nilianza kwenye arobaini na mbili? La, nilianza kwenye thelathini na tano. Thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini, arobaini na moja, arobaini na mbili. Arobaini na mbili? Sasa, iko hapa mahali fulani, ama inapaswa kuwa. Arobaini na mbili, B, arobaini na mbili.

154 Angalia kote kwa jirani yako, huenda ni kiziwi sasa, wala hawezi kusimama, mnaona, hanisikii. Arobaini na mbili, B, arobaini na mbili. Labda walitoka nje. Arobaini na tatu, B, arobaini na tatu. Hapa. Arobaini na nne, arobaini na tano. Inueni mikono yenu, ndipo ninaweza kukuona kwa urahisi. Arobaini na tano. Huko nyuma kabisa, sawa. Arobaini na tano, arobaini na sita. Hapa. Arobaini na saba. Vema, bwana. Arobaini na nane. Papa hapa. Arobaini na tisa. Hilo ni jema. Vema, hamsini. Huko nyuma kabisa pembeni. Vema.

155 Sasa, kusudi tusininii. . .Sasa, huenda tukaweza kufikia zaidi ya hii. Sasa nataka kila mtu humu ndani ambaye hana kadi ya maombi, nawe ni mgonjwa, kuinua mkono wako, usiye na kadi ya maombi. Vema.

156 Vema, sasa angalieni, sasa, wakati wanapowakusanya pamoja, nisikilizeni sasa. Sasa, mtu yeyote ashikwe na wasiwasi, na tafadhali usiondoke jengoni, tafadhali. Kaa tu kimya, kimya kabisa. Sasa, katika dakika kumi na tano tutakuwa tumetoka, kama mtatulia tu, kimya kabisa. Mnaona, wakati Roho Mtakatifu. . .

157 Ni wangapi walioona picha Yake sasa? Tunayo kote nchini. Iko kote ulimwenguni, imetundikwa huko Washington, DC, Nguzo ya Moto ambayo George J. Lacy, mkuu wa FBI, alama za vidole na hati, aliipiga picha hiyo na kuichunguza kuingizwa mwanga maradufu na kadhalika, alisema, "Nuru iligusa lenzi," na kutia sahihi hati ya kiapo kwa ajili yake. Kasema, "Si saikolojia, kwa sababu jicho la ki—kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia."

158 Sasa, tuseme hiyo ni Nguzo ile ile ya Moto. Ni wangapi wanaojua ya kwamba ile Nguzo ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli nyikani ilikuwa ni Kristo? Hakika, ilikuwa. Yule Malaika. . .Vema, alipokuwa hapa, Yeye alisema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Hiyo ni kweli? Vema, basi wakati alipokuwa hapa duniani katika mwili wa nyama, mnaona kile alichokuwa?

159 Sikilizeni, kimya kabisa sasa, m—mtalikosa. Mnaona kile alichofanya alipokuwa hapa? Alijitangaza Mwenyewe kuwa Masihi. Hiyo ni kweli? Tuliyapitia tu. Sasa, Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, nitakuwa pamoja nanyi. Nilitoka kwa Mungu, ninaenda kwa Mungu." Ni wangapi wanajua Maandiko yanasema hivyo? Vema basi, Yeye alitoka wapi? Hiyo Nguzo ya Moto, hapa chini na kukaa katika mwili, kisha akarudi kwenye hiyo Nguzo ya Moto. Mnaamini hilo ndilo alilofanya?

160 Mbona, Paulo, ama Sauli, hasa, akishuka kwenda Dameski, alikuwa akienda zake, ndipo nuru kuu ikamulika mbele yake, na—na kumwangusha chini na kuyapofusha macho yake. Hiyo ni kweli? Naye akasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu." Hiyo ni kweli?

161 Wakati Petro alipokuwa gerezani, ni kitu gani kilichoingia kwenye seli na kwenye nguzo, na kufungua milango na kumtoa nje? Nuru, Nguzo ya Moto. Basi kama Nguzo iyo hiyo ya Moto tuliyo nayo. . .

162 Ulimwengu wa kisayansi unajua ni kweli. Bw. Lacy alisema, anapaswa kujua, yeye ni mtu wa serikali, mkuu wa FBI, alama

za vidole na hati, za alama za vidole, na kadhalika, akasema, "Hakujawahi kuwa na picha iliyothibitishwa kisayansi ya kwamba kuna Kiumbe cha kimbinguni." Sasa, hiyo ni kweli. Iko moja kwa moja kwenye hati yake. Tunayo papa hapa. Moja yazo imetundikwa kwenye ukumbi wa sanaa wa kidini huko Washington, DC, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha.

163 Ndugu Arganbright alikuwa pamoja nami (Papa *hapa*. Ni wangapi wanaomjua Ndugu Arganbright? Mtu mzuri, mwaminifu.), amesimama pale pale (Hiyo ilikuwa wapi, Ndugu? Ilikuwa Ujerumani?) huko Lausanne walipotaka kujua kama, kamera ile ya Kijerumani ingeipiga picha. Nikasema, "Labda itaipiga."

164 Kwa hiyo nilipomhisi akija, kulikuwa na mtu aliyefanana na kasisi, amesimama pale, Roho Mtakatifu akaanza kumwambia alikuwa kiongozi wa wakomunisti, na kumwambia alikuwa na ugonjwa wa tumbo, na kadhalika, wakaanza kupiga picha, nao wakaipiga picha ikishuka, wakati ilipotia mafuta, na wakati iliporudi na kuondoka, kamera za Kijerumani. Loo, wanazo kila mahali. Kwa hiyo ulimwengu wa kisayansi, kama nikifa usiku wa leo, ulimwengu wa kisayansi unajua hiyo ni kweli, inatoka kwa Mungu.

165 Kanisa kote ulimwenguni linajua inatoka kwa Mungu, kwa sababu ina ishara zile zile ilizofanya ilipokuwa ikikaa katika Bwana wetu Yesu. Nasi ni wana na binti za Mungu kwa kufanywa wana wenye mamlaka kupitia Yeye, na Roho Wake aliyekuwa ndani Yake yuko ndani yetu. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Kila mtu anaelewa dhahiri kabisa?

166 Sasa, hebu nione tena, ninyi msio na kadi za maombi mlio na maradhi na magonjwa, nawe unataka Mungu akuponye, sijali uko wapi, inueni mikono yenu. Vema, hiyo ni karibu kila mahali. Sasa, iweni na kicho kabisa, msipige kelele hata kidogo, iweni na kicho kabisa. Dumu tu mtamu sana nafsini mwako, nawe ufanye hivi: Useme, hebu nikupe Andiko dogo sasa, useme, "Bwana, mimi ni kama yule mwanamke aliyejipenyeza katikati ya umati. Wakati alipoona na kutambua, alikuwa ametokwa na damu, alikuona Wewe, naye akasema, moyoni mwake, 'Kama nikiweza kugusa vazi la Mtu huyo, nitapona.'"

167 Mnakumbuka hadithi hiyo? Na, labda, hakuwa na kadi ya maombi. Lakini alitaka kupitia kwenye huo umati, naye akajipenyeza. Kwa hiyo akaligusa vazi Lake, hilo lilikuwa ni vazi linalopwaya sasa, vazi la Kipalestina, kamwe asingeuhisi kimwili, kwa sababu ilithibitishwa, alimgusa namna *hiyo*, kisha akarudi, akaketi chini. Akageuka, na kusema, "Ni nani aliyenigusa?"

168 Naye Mtakatifu Petro mashuhuri akasema, akamkemea, kwa maneno mengine, huenda alisema hivi: "Unamaanisha nini

kwa kusema kitu kama hicho? Mbona, hilo ni—hilo ni swali la kipumbavu! Kwa nini useme kitu kama hicho? Vema, kila mtu amekukumbatia, na kukupa mkono, na kusema, 'Rabi, tunafurahi kukuona.' Vema, kwa nini uulize kitu kama hicho?" Mnaona, hivyo ndivyo watu wanavyofanya siku hizi.

Akasema, "Lakini huu ulikuwa ni mguso tofauti, naona kwamba nimekuwa dhaifu."

169 Sasa, kama mguso mmoja kama huo ungemfanya Mwana wa Mungu dhaifu, ungenifanya nini mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Kwa sababu tafsiri niliyowapa muda mfupi uliopita, "Mambo haya nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya, na *mengi* kuliko haya." Yeye ndiye Nguvu zangu. Mnaona? Lakini inakufanya dhaifu. Danieli aliona ono moja, akafadhaika kichwani mwake kwa siku nyingi. Mnaona? Sasa, Yeye aligeuka, akaangalia mpaka akapata, ndipo akamwambia shida yake ilikuwa ni nini, naye akaponywa.

170 Sasa, kwa wahudumu hawa, nadhani, walioketi hapa jukwaani, ndugu zangu, na katika kusanyiko, ni wahudumu wangapi, hapa usiku wa leo, wamesoma Maandiko kwamba Yesu Kristo, sasa hivi, ni Kuhani wetu Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Ni wangapi wanajua hilo? Vema. Vema basi, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, basi ingembidi kutenda vile vile kama alivyotenda jana, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule. Hiyo ni kweli? Maana Mungu hawezi kubadilika. Mnaona?

Vema, sasa, kama utakuwa tu, usi—usishikwe na wasiwasi, mtu yeyote asiinuke, tulieni tu, wala hutakuwa na wasiwasi, na utaangalia tu kwa utulivu.

Ukisema, "Ndugu Branham, naweza kuja nikuguse?"

171 Hilo lisingekuwa bora kuliko kuigusa ile benchi *pale*, haingekufaa zaidi ya kuigusa hiyo, kunigusa mimi. Mimi si ninii, si kitu mimi, mimi ni mwenye dhambi duni tu, aliyeokolewa kwa neema ya Mungu. Mguse mumeo, mguse mkeo, mguse ndugu yako, mguse mtu mwingine, ni mamoja tu, unamgusa mwanadamu.

172 Sasa, haileti tofauti yoyote kama nimeweka mikono yangu juu yako au la, bali mguse tu Yeye wakati mmoja. Mguse tu, na uache Uhai Wake uliofufuka ulio miongoni mwetu sasa, uone atakalofanya. Angalieni kama Yeye si Kuhani Mkuu yeye yule bado.

173 Ndugu, kama Yeye—kama Yeye atafanya hivyo, inaonekana kana kwamba inapaswa kuondoa kila wazo potovu moyoni mwako. Sivyo? Inaonekana kana kwamba ni kamilifu sana, hilo hapo Neno linalolisema. Unaona?

174 Sasa, kitu pekee kinachokuzuia usilipokee ni uzito mkubwa mno, ukisema "Loo, laiti angeenda nyumbani, nimechoka sana.

Loo, na—najisikia vibaya sana, laiti angeondoka." Unaona, kamwe hutapata chochote.

175 Huna budi kuwa macho, ukiangalia, ukiangalia kwa uchaji, ukiamini, "Bwana, hii ndiyo saa yangu. Naja, Bwana, jalia nikuguse Wewe, mtu huyo hanijui."

176 Ni wangapi huko nje ambao ni wageni kwangu? Inua mkono wako, unajua ya kwamba sikujui. Ni wangapi kwenye mstari wa maombi ambao mimi ni mgeni kwenu, ambao siwajui? Inua mkono wako. Kila mmoja. Kote kwenye kusanyiko, hakuna mtu mmoja humu ndani sasa hivi ninayemwangalia, ama mahali popote ninapoweza kuona, ninayemjua, hata mmoja.

177 Huku nyuma mtu pekee ninayemjua ni mwanangu mwenyewe aliyesimama pale, Ndugu Arganbright hapa, huyu mhudumu hapa, nimepeana mikono na ndugu huyu hapa, katibu wangu wa huduma, na mmoja wa mameneja aliyeketi papa hapa, hao ndio watu pekee katika jengo hili ninaowajua. Na kama wana shida yoyote, sitazungumza nao. Nitaliachilia, kama tulivyoingia chumbani jana usiku, kule nyuma, nitaachilia hilo liendelee mpaka wakati huo.

178 Lakini sasa, sasa tume—tumezungumza juu yake, tumehubiri juu yake, tumelitangaza kwa Neno. Ni wangapi wanajua. . .anayesema, "Neno linasema hivyo"? Hebu tukuone. . .Ni wangapi wanasema ya kwamba "Tunaamini ya kwamba Yesu alimaanisha yale hasa aliyosema, kwamba Malaika huyo angerudi duniani kwa Kanisa teule"?

179 Sasa, "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu," asiyeamini ataondoka na kutikisa kichwa chake, "La, bwana." Lakini Yeye—Yeye hakutumwa kwake, alitumwa kwa mwaminio, kama Ibrahimu. Kamwe hakushuka kwenda Sodoma, Yeye alienda kwa Kanisa teule, Kanisa lililoitwa litoke, Kanisa lililotengwa, Naye akawaonyesha ishara hiyo. Kama alivyokuwa wakati huo, Yesu alisema jambo lilo hilo lingetukia.

180 Sasa, ni wangapi wanaoamini ya kwamba hiyo ni kweli, ndiyo saa? Sasa, kama Yeye atakuja, na atawafanyia jambo fulani watu hawa hapa kama tu alivyofanya wakati huo, huku kwenye kusanyiko hapa, na karibu na hili, popote pale, kama Yeye atafanya jambo lile lile, ni wangapi watakaoahidi kwamba "Kwa imani yote niliyo nayo nitamkubali"? Inua mkono wako, kila mmoja anayetaka kuninii. . .Mnaona, ninajaribu kupata mahali hapo.

181 Sasa, hebu na tuimbe kwa upole kwa muda kidogo tu, *Amini Tu,* kama wewe, Dada, utatupa sauti yake:

> Amini tu,

Kila mtu awe na kicho sasa, iweni katika maombi.

> . . .amini,
> Mambo yote yanawezekana, amini tu;

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, amini tu.

182 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninachukua kila nafsi hapa ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Msisogeesogee, iweni na kicho kabisa. Vema, anza ninii yako . . .

Mwaweza tu kusogea karibu zaidi?

183 Sasa, kwa wasikilizaji: Sasa, nimekuwa nikihubiri kwa hiyo ninataka kuzungumza na mwanamke huyu. Sasa hebu niliwekee msingi Kimaandiko sasa, kwenu, hebu na tuchukue mahali nilipokuwa nikizungumzia, hebu tuone, ni Yohana Mtakatifu 4. Hawa hapa mwanamume na mwanamke. Ninaamini mliinua mikono yenu kwamba hatufahamiani. Hatufahamiani. Ili kusanyiko huko nyuma kabisa lijue ya kwamba hatufahamiani, sote wawili tutainua mikono yetu juu kwamba hatufahamiani.

184 Sasa, hii ni kama tu Yohana Mtakatifu 4. Bwana wetu alikuja kisimani, na kukutana na mwanamke, kamwe hakuwa amemwona, kamwe hakuwa amemwona Yeye, bali Yeye alielezea jinsi hali ya mwanamke huyo ilivyokuwa, mahali shida yake ilikuwa. Na, upesi, mwanamke huyo akasema, "Hapana shaka wewe ni nabii. Tunajua yuaja Masihi, na Masihi ajapo Yeye atatuambia mambo haya." Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli?

185 Na sasa, Dada, ndiyo kwanza nimalize kusema, ninaamini, ya kwamba—ya kwamba alikuwa akienda Zake Yeriko, lakini ilimbidi kupitia Samaria, naye Baba akamtuma huko juu. Vema, sasa, kama hatufahamiani, sijawahi kukuona, wala hujawahi kuniona, na hii ni mara yetu ya kwanza kukutana, basi . . .

186 Ninaamini Mungu alinituma huku chini. Ndugu Arganbright pale alinipigia simu, na kuniomba kama ningekuja Long Beach, na pia nije kwa Ndugu Arnie Vick. Nikamwambia nitakuja. Vema, wakaweka majuma yote mawili hapa chini kwa sababu fulani, basi ninaamini huyo alikuwa ni Mungu akifanya hivyo.

187 Ndiposa mimi nipo hapa, ndiposa wewe upo hapa. Baba alinituma hapa, bali mimi sikujui wewe. Kwa hiyo kama Masihi angetokea kuninii . . . Mimi nikiwa mwanadamu, mwanadamu, Ndugu yako Branham, sijui lolote kukuhusu, Mungu anajua hilo, na Neno Lake hapa. Lakini kama Masihi atakuja na kunitia mafuta, basi angefanya jambo lile lile alilofanya kule chini, angejua shida yako ilikuwa ni nini, na angeweza kukwambia.

188 Sasa, vipi kama—kama Yeye angekuwa amesimama hapa Mwenyewe, binafsi, sio mimi, bali Yeye? Ungesema, "Ee Bwana Yesu, niponye."

189 Sasa, Yeye asingeweza kufanya hivyo, angesema, "Mtoto wangu, tayari nimefanya hivyo nilipokufa kwa ajili yako." Lakini basi Yeye angesema, "Upate kujua ya kwamba Mimi

Ndiye, nitafanya kama nilivyofanya nilipokuwa hapa duniani, kwa sababu siwezi kubadilika. Unaona? Sasa, kama Baba atanionyesha shida yako ni nini, basi ungeniamini mimi kwamba ni Masihi?"

Ungesema, "Naam, Bwana." Na labda angefanya jambo lile lile alilofanya, maana ingembidi kufanya hivyo, Yeye—Yeye ni yule yule.

190 Lakini unaona sasa, Yeye Mwenyewe, ule mwili, Yesu Kristo, ameketi mkono wa kuume wa Mungu Mbinguni, bali alimtuma tena Roho Mtakatifu, yule Roho aliyekuwa juu Yake. Sasa, alikuwa Naye bila kipimo, utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikuwa ndani Yake. Mimi nina kijiko kidogo tu, hicho ndicho tulicho nacho, ninacho kwa kipimo. Lakini kama nikichota kijiko kimoja cha maji kutoka baharini, na kuyaleta hapa juu na kupima kemikali zilizomo, kemikali zile zile za bahari nzima zimo kwenye kijiko hicho, ila tu si kiasi hicho.

191 Mnaona, ninapozungumza, ninaangalia kitu fulani. Unajua ya kwamba jambo fulani linaendelea. Sasa, kama wasikilizaji wanaweza kuona jambo hilo, Nuru mnayoiangalia kwenye ile picha imesimama kati yangu na mwanamke huyo. Ile *pale*. Sasa, inanifanya nijisikie vizuri, ninajua Yeye yupo hapa, nilikuwa na hofu kidogo kwanza, bali Yeye yupo hapa sasa. Unajua ya kwamba jambo fulani linaendelea. Ninataka ushuhudie kusanyiko kama ndivyo ama sivyo, muda mfupi tu uliopita hisia tamu sana, ya starehe ilikuja, hisia nzuri tu, ya starehe. Hiyo ni kweli, sivyo?

192 Sasa, kama Bwana Yesu atanijulisha jambo fulani kukuhusu, ambalo, sijui chochote, lakini kama angeweza kuniambia jambo fulani ambalo umekuwa, ama kitu kama hicho, angeweza kukwambia kile umekuwa, Yeye angejua utakavyokuwa, kama angeweza kukwambia hilo, wewe ungekuwa mwamuzi kama ni kweli ama si kweli.

193 Unasumbuliwa na kitu fulani kwenye nyonga yako, naamini, kuna kasoro kwenye nyonga yako, hiyo ndiyo unayotaka niombee. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili watu waweze kuona.

194 Vema. Unaamini sasa kwa moyo wako wote? Sasa hebu kidogo. Unaona? Ili kwamba usininii...utaelewa kabisa haikuwa ni kubahatisha. Lakini hivyo ni kadiri Yesu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli. Lakini sasa ili kukufahamisha tu ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake: Hilo linathibitisha jambo hilo.

Unasema, "Huenda ikawa ilikuwa ni kubahatisha, Ndugu Branham."

195 Ningewezaje kubahatisha hilo, wakati, sasa hivi, sikujua nilichomwambia? Ingebidi itoke kwenye kanda. Sasa iweni na kicho.

196 Angalieni tu tena, kwa ajili tu ya ono, hivyo tu, ninakuangalia, naam, ninakuona ukirudi nyuma, nyuma, nyuma, naam, ni—ni kwenye nyonga yako. Vema, una shida ya nyonga.

197 Nawe una mtu mwingine moyoni mwako ambaye unamwombea, huyo ni mwana. Ana kasoro, amefungwa plasta ngumu. Hiyo ni kweli. Halafu kuna jambo lingine, mvulana huyo ametiwa uvuli, hiyo inamaanisha ya kwamba a—anahitaji wokovu, yeye si Mkristo. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Ingekusaidia? Vema, ingekusaidia? Bibi Morris. Nenda ukaamini.

Sasa, unamwamini Bwana Yesu Kristo? Sasa, inueni tu mikono yenu, na kusema, "Asante, Bwana Yesu."

198 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe hujatuacha peke yetu, Wewe umetubariki na kutupa wema Wako. Ninaomba ya kwamba utatusaidia kuamini sasa, na kila mmoja aponywe. Kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu, tunaomba. Amina.

199 Sasa tafadhali ketini, tafadhalini, tafadhalini. Msisogee, ketini kimya. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho. Ni wangapi wanaojua hilo? Hakika. Angalieni hapa, *hiki* ni nini? Kidole changu. *Hiki* ni nini? Mkono wangu. *Hiki* ni nini? Sikio langu. Lakini *mimi* ni nani? Mnaona? Ni yangu, mimi, ndani. *Hii* ni mali yangu. Hilo ndilo ninalozungumzia, *wewe*, roho yako. Na kwa kutiwa mafuta sasa na Roho Mtakatifu Wake, ninawasiliana nanyi. Ombeni, ombeni, msiwe na shaka. Ingekuwaje sasa hivi kama kanisa lingekuwa hai?

200 Je, huyu ndiye mtu anayefuata? U hali gani, mama? Hatufahamiani, pia, nadhani. Sikujui, lakini Mungu anakujua. Na kama Yeye anakujua, basi njia pekee ningeweza kukujua ingekuwa ni kwa kitu fulani Yeye angeniambia.

201 Yesu alisema, "Ninafanya tu kama vile Baba anavyonionyesha." Mnaona? Na hiyo ndiyo njia pekee ningaliweza kufanya, kama tu vile Baba angeonyesha. Lakini kama atanionyesha shida yako ni nini, utamwamini?

202 Yule mama mweusi aliyeketi pale, papa hapa nje, akiwa na shinikizo kuu la damu, unaamini Yesu Kristo anakuponya sasa? Uligusa Kitu fulani, sivyo? Vema. Umeponywa sasa, Yesu Kristo amekuponya.

203 Sasa, niambieni aligusa nini, niambieni aligusa nini. Alimgusa Kuhani Mkuu. Simjui mama huyo, sijawahi kumwona. Lakini niligeuka hapa, nilijua *huyu* alikuwa ni mwanamke mzungu, kisha nikaangalia, kulikuwa na mama mweusi amesimama *hapa*. Nikaangalia kote, alikuwa amevaa kitu

kidogo kilichoonekana cha kiajabu-ajabu kichwani mwake, nikawaza, "Iko wapi?" Nikaihisi ikienda, kama mapigo ya moyo, ikifanya "*chu*, *chu*, *chu*, *chu*," nikaangalia, hiyo hapo, nikaona ikilegea namna hiyo. Nikawaona wakiweka kitu fulani mkononi mwake na kukisukuma, ndipo Yeye akasema "Shinikizo kuu la damu."

Imekwisha sasa, Dada, Yesu Kristo alikuponya.

Je, Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu?

204 Sasa iweni na kicho sana sasa. Tunataka . . . Mungu anaabudiwa, tunapenda kumwabudu, bali Roho Mtakatifu ni mwoga sana, nyamazeni tu kabisa. Sasa ninyi jamaa wadogo iweni wazuri sana, hapa chini sasa, mbele, wazuri sana sasa, watulivu sana.

205 Kila mtu aanze kuomba sasa, akisema, "Baba, mimi ni mhitaji," wakati nikizungumza na mwanamke huyu hapa, kwa sababu ni rahisi zaidi kuwasiliana naye. Sisemi angemwambia chochote, lakini asipomwambia . . .

206 Asipokwambia jambo moja, kama nikipita tu karibu nawe na kukuwekea mikono, unajua hapana budi kuwe na namna fulani ya upako hapa. Hiyo ni kweli? Nisingejua mambo haya. Vema basi, kama unaamini kwamba ni Roho Mtakatifu, utapata thawabu yako; kama ukiita Hiyo kitu kingine, hiyo ingekuwa kati yako na Mungu, unaona, nisingejua. Ninaweza tu kutangaza kwamba Biblia inasema jambo hilo, Hili hapa kukithibitisha.

207 Sasa, dada yetu aliyesimama mbele yangu, anaugua u—ugonjwa wa wasiwasi, na koo lake lina kasoro. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

208 Unaamini? Ninaangalia tu sasa. Ninaamini ingekuwa afadhali kama nikichukua tu wakati wangu pamoja na wachache wao namna hiyo, na kuiangalia tu, nafikiri itashikilia kusanyiko vizuri zaidi kuliko kuanza tu kushughulikia umati mkubwa. Sasa iweni tu na kicho kabisa, ninajisikia kuongozwa kufanya jambo hili.

209 Kuna kitu kingine moyoni mwake, yeye hajaninii—hajajifungua bado, kuna jambo lingine hapa. Naam, ninaona ni kitu gani, ni shida ubavuni mwako. Ni kivimbe, sivyo? Unaamini Mungu anaweza kuniambia kiko upande gani? Upande wa kushoto. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini sasa?

210 Kuna kitu kingine moyoni mwako, hicho ni mwanamume. Mtu huyo ni mume wako, ameketi huko nje. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Utaamini kwa ajili yake, na kuweka leso hiyo juu yake? Ana shida ya macho yake, na ya masikio yake. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Nenda, weka leso hiyo juu yake, apone katika Jina la Yesu Kristo.

211 Aminini sasa, aminini. Sasa kitu hicho chote kinakuwa kama Nuru kote jengoni namna hii, kwa hiyo sasa iweni na kicho kabisa. Na kama sitawaona baada ya hili kwa kitambo kidogo, vema, tutawaona kesho usiku. Sasa iweni na kicho kabisa, kila mtu sasa, na mjaribu kusaidia, kufanya kazi pamoja nami. Mnatambua . . . Kama mtu yeyote anataka kuja, kuchukua mahali pangu, unaweza kuja moja kwa moja, unaona, unaona. Lakini iweni tu na kicho kabisa, sasa aminini.

212 Nipo hapa . . . Mimi si mhubiri, si—sina elimu ya kuwa mhubiri. Mungu alinipa . . . alinifanya kitu kingine, mnaona, ili niweze kuwasaidia. Mchungaji wenu anaweza kuwahubiria na kuwasaidia, bali Yeye—Yeye alinipa hii nipate kuwasaidia, maana ninawapenda, na Yeye anawapenda, Yeye anataka nionyeshe upendo Wake kwenu.

213 U hali gani? Sasa, hii hapa picha nzuri tena, dada m—mweusi na mzungu. Sasa, hivyo ni kama ilivyokuwa kule Samaria, Myahudi na Msamaria. Lakini Yesu alimjulisha upesi, kasema kwa sababu tulilelewa katika sehemu tofauti ya nchi, basi iligeuza ngozi zetu rangi tofauti, Mungu ni Mungu wa jamii zote.

214 Yeye, kama tu tuta la maua, Yeye ana maua meupe, na maua mekundu, na maua ya samawati, na hilo ndilo shada Lake, mnaona. Yeye—Yeye hutufanya hivi, bali mioyo yetu, sote tunatoka kwa mtu mmoja, Adamu na Hawa. Hiyo ni kweli. Nchi tulimoishi, ilibadilisha rangi yetu, haina uhusiano wowote na roho na mioyo yetu. Hiyo ni kweli. Mungu ni halisi tu kwako kama alivyo kwa mtu mwingine yeyote. Unaamini hilo? Na unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini mambo ambayo nimesema? Najua unaamini.

215 Ndio kwanza nitoke Afrika hivi majuzi, miaka michache iliyopita, ninarudi tena, pia. Loo, kuona imani hiyo, imani hiyo rahisi!

216 Kama Mungu atanifunulia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Utaamini, na atujalie. Ugonjwa wa rektamu, ni rektamu.

Sasa, ninyi nyote watu weusi aminini sasa; huyu ni dada yenu.

217 Ngoja, kitu zaidi ya hicho, pia. Alisema ilikuwa ni ugonjwa wa matumbo, matumbo, nayo yanasinyaa, yanasinyaa, yanakunjana, matumbo. Hiyo ni kweli. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Kama nikikwambia jina lako ni nani, ungeniamini vizuri zaidi? Wasikilizaji wangeamini vizuri zaidi? Mngeamini? Bibi Jefferson, nenda nyumbani, Yesu Kristo anakuponya. Mungu akubariki.

Mwaminini Mungu.

218 U hali gani? Hatufahamiani. (Niambieni nitakapofikisha watatu hivi, ndipo basi nitaninii . . .) Hatufahamiani, sikujui wewe, hunijui mimi. [Dada huyo anasema, "Nimekuwa kwenye mikutano yako."—Mh.] Mama? ["Nimekuwa katika mikutano yako . . .? . . . "] Umekuwa katika mkutano wangu, bali nisingekujua, wewe uliketi tu kwenye kusanyiko. Vema.

219 Jambo fulani lilitukia, bali nililikosa. Ilikuwa kwenye hiyo kona, labda ilikuwa ni huyo mama. Huyo mama ambaye ndio kwanza aketi chini, hivi wewe ndiye mama ambaye ndio kwanza aombewe, ama kitu fulani? Naam. Ni—niliitazama Nuru hiyo, ikaondoka jukwaani, bali nilifikiri ilikuwa ni mwanamume. Ni mwanamume, aliyeketi pale pale, ana ugonjwa wa koo. Naam. Naam, bwana. Huyo mtu aliyeketi karibu nawe ana furaha sana, maana ndiyo kwanza aponywe, utukufu wa Mungu juu yake. Mtu huyo alikuwa na ugonjwa wa koo. Ugonjwa wako wa koo umekuacha, bwana. Rafiki yako aliyeketi hapo akikuombea alishusha nguvu za Mungu juu yako. Nenda sasa, dhambi zako zimesamehewa, koo lako limepoywa. Nenda ukaponywe, katika Jina la Bwana Yesu.

Ninawapa changamoto: Mwaminini Mungu.

220 Mama huyo aliyeketi nyuma hapo, akiniangalia moja kwa moja awezavyo, hivi hamwoni hiyo Nuru imesimama juu yake? Anaugua ugonjwa wa kibofu. Unaamini kwa . . .? Simama, Dada, simama na ukubali uponyaji wako. Vema, endelea mbele, Yesu Kristo anakuponya.

221 Sijawahi kumwona huyo mwanamke maishani mwangu. Hivi hatufahamiani? Inua mkono wako, mama, kama hiyo ni kweli. Vema. Nenda nyumbani, ukawe mzima. Ulipoketi chini, kuna mama aliyeketi papo hapo karibu nawe hapo, anayesumbuliwa na ugonjwa wa koo, pia. Simama, mama, na ukubali uponyaji wako. Hatufahamiani. Nenda nyumbani, ukawe mzima, Yesu Kristo anakuponya.

222 Hivi hamwezi kuona ya kwamba Yeye yu hai? Kristo yu hai, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mwaminini tu Mungu, enyi watoto, mwaminini Mungu. Usitie shaka, amini tu kwa moyo wako wote. "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

223 Una ugonjwa wa wasiwasi, kikohozi. Mishipa yako ndiyo inayokufanya ukohoe. Unahofu kuna kasoro kooni mwako, bali sivyo. Unaposhikwa na wasiwasi, hapo ndipo unapokohoa zaidi. Hilo silo jambo lako kuu, hata hivyo, unamwombea mtu mwingine. Alipata ajali, sivyo? Mwanao, hospitalini, amepoteza fahamu nusu. Unahofu kama angekufa, ama kitu fulani, yeye—yeye ameokoka, lakini unaogopa kidogo hakuomba vizuri. Hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ni vema, ni sawa, endelea, atatoka katika hali hiyo ukiamini kwa moyo wako wote, na usitie shaka, amini.

224 Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Hilo huwashangaza watu ninaposema hivyo. Mimi sidai kuwa nabii, mimi ni ndu-. . . Mimi ni—mimi ni mtumishi Wake, ndugu yenu.

225 Hebu kidogo, kidogo tu, jambo fulani lilitukia mahali fulani katika kusanyiko. Iweni na kicho sasa, jambo ndilo hilo, iweni na kicho kabisa na mwombe sasa, nyosha tu mkono na kusema, "Bwana Yesu," sijali unachohitaji, sema, "mtu huyo hanijui. Sina kadi yoyote ya maombi, sitakuwa kwenye mstari huo wa maombi, yeye hanijui, lakini, Bwana, kama utaniruhusu tu niguse vazi Lako, halafu Wewe umwelekeze kwangu." Mnaona? Angalia tu kama hiyo si kweli. Ninii tu, sasa iweni na kicho kabisa.

226 Hatufahamiani, hatujuani mmoja na mwenzake. Kama hiyo ni kweli, vivyo hivyo tu, tunainua mikono yetu, watu waone. Vema. Hatufahamiani, basi, bali Mungu anatujua sote wawili. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Sasa, sababu ya mimi kusema hivyo, Yeye aliniambia. . . Umesoma, labda umesoma kitabu changu, umewahi kusoma hicho kitabu? Alisema, "Ukiwafanya watu wakuamini." Kuamini nini? Sio kuniamini mimi kuwa ni Yeye, bali kuamini ya kwamba Yeye alinituma. Unaona? Hana budi kumpata mtu fulani, mahali fulani. Unaona?

227 Kwa hiyo Yeye ana watu wengine hudumani, watu mashuhuri, mimi ni mmoja wa walio wadogo. Lakini sehemu yangu ndogo, ninapenda kumfanyia Yeye, kumwonyesha Yeye onyesho langu kuhusu upendo wangu Kwake, kuwa na kicho. Ninampenda kwa moyo wangu wote. Nami siwezi kumpenda Yeye pasipo kuwapenda ninyi nyote. Mnaona? Kwa kuwa angependa niwapende ninyi nyote kuliko kumpenda Yeye; afadhali mngewapenda watoto wangu badala ya kunipenda mimi. Nami, nikiwa mzazi, ninawazia hivyo, na Yeye je?

228 Sasa, mnasema, "Ndugu Branham, unafanya nini?" Ninangojea kuona yale atakayoniambia. Kama hataniambia chochote, nami nije tu nikuwekee mikono, ungeamini, kwa vyovyote vile? Utaamini, kwa vyovyote vile.

Je, kusanyiko lingeamini hivyo, hata hivyo? Hiyo hapo inakuja, hata hivyo.

229 Umefanyiwa upasuaji, mbaya sana, haufanyi vizuri, unaogopa. Unaogopa kansa sasa. Unaamini Yeye anaweza kuniambia huo upasuaji ulikuwa ni nini? Ninaona upasuaji, ilikuwa ni kibofu nyongo, naamini, hiyo ni kweli. Unaogopa. Nisiposema chochote, ni kitu gani, ama kama ndiyo, kama Mungu atakujalia tu uwe na imani, hilo tu ndilo unalohitaji, sivyo? Hiyo ni kweli?

230 Kama ataniambia wewe ni nani, ama unakotoka, ama kitu kama hicho, ama kitu kingine maishani mwako, utaamini? Je,

ingekufanya uamini kweli . . . ? Unajua ya kwamba sikujui. Wewe hutoki hapa, unatoka mahali panapoitwa Downey. Wewe ni Bibi Kelly. Sasa rudi, umeponywa, Yesu Kristo anakuponya.

Unaamini? Mwamini Mungu, usiwe na shaka.

Mwanamke huyo, je, huyo ndiye yule mwanamke ndiyo kwanza aponywe, ama kuombewa? Nuru hiyo ilikuwa papo hapo muda mfupi tu uliopita, papo hapo alipokuwa.

231 Mtu fulani anaomba. Kijana, una kadi ya maombi? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, mtumishi Wake? Unaamini Mungu atamponya rafiki yako? Kama nitakwambia kuna shida gani, utaamini? Kansa. Kuwa na imani na uamini sasa, atapona. Amina.

232 Mama aliyeketi papa hapa nyuma akiniangalia, una shida ya mguu wako, ilisababishwa na upasuaji, uliyevaa miwani, nywele za kahawia. Unaamini kwa moyo wako wote? Inua mkono wako. Vema, unaweza kwenda nyumbani na kuwa mzima, Yesu Kristo alikuponya.

Unaamini, bwana? Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe. Amina. Amini sasa, usiwe na shaka.

233 Mama, jicho lako lina kasoro. Kama nitakwambia ni nini, utaamini? Ni kansa. Utakubali uponyaji wako? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

Kila mtu aombe sasa, iweni na imani.

234 Jamani, hii hapa nyingine, kansa. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, Dada? Njoo, hebu nikuwekee mikono wakati upako . . . Nenda sasa, na Mungu wa Mbinguni na akuponye na kukupa afya.

235 Ugonjwa huo wa figo ulikuacha ulipokuwa umeketi pale. Nenda ukaponywe. Mwamini Bwana Yesu kwa moyo wako wote. Usitie shaka, amini tu kwa moyo wako wote. Vema.

236 Njoo, mama. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo. Hivi huamini hilo? Unaamini wako uliponywa? Basi nenda zako, na kusema, "Asante, Bwana Yesu," na upate afya.

Ulikuwa na ugonjwa wa wanawake, na pia ugonjwa wa moyo. Unaamini umekwisha? Vema, nenda zako, na useme, "Asante, Bwana," uponywe.

237 Mwanamume wa umri wako anapaswa kuwa na maskini tezi dume, ugonjwa wa fadhaa, lakini moja ya mambo yako makuu ni mwuaji, huo ni ugonjwa wa moyo. Unaamini ya kwamba Yeye atakuponya? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Nenda ukapate afya, Yesu Kristo anakuponya.

238 Njoo ukiamini sasa. U hali gani, mama? Wewe ni mwembamba sana, bali una kivuli juu yako, umetiwa uvuli

wa mauti. Ni kansa, mwuaji. Unaamini Mungu atakuponya? Nenda.

Nami ninamkemea ibilisi huyo kutoka kwa dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, Shetani, toka kwake.

Mimi ni mgeni kwako, mama. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Ungeamini?

239 Ngoja kidogo. Unayeketi papo hapo na ugonjwa wa tumbo, bwana, unaamini Mungu anakuponya? Unaamini kwa moyo wako wote? Mtu mwenye nywele nyeusi, jamaa mdogo aliyevaa shati jeupe, akiomba hapo na. . .Sasa, jambo ndilo hilo. Nenda nyumbani, na ule sasa, ni tumbo lenye wasiwasi, lilikuwa limekuziba. Unamwamini Yeye kwa moyo wako wote? Unakubali uponyaji wako? Simama, kama unaamini, simama tu moja kwa moja. Vema, nenda nyumbani, Yesu Kristo anakuponya.

240 Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini, utaniamini, ningekuwa nabii Wake, mtumishi Wake? Kisukari chako kitakuacha, kama utaamini. Nenda nyumbani, uwe mzima, Yesu Kristo atakuponya.

241 Mama, una shida kadhaa, hiyo ni kweli, kwa kuwa mama wa umri wako kweli angekuwa na hayo. Lakini jambo unalotaka niombee ni ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Una moyo dhaifu, wenye wasiwasi. Unapolala, inakuwa mbaya zaidi kuliko wakati wowote. Kwa hiyo sasa kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima, Yesu Kristo anakupa afya.

242 Vipi kuhusu kuamini? Unayeketi hapo kwenye kiti hicho cha nje, siwezi kukuponya. Una kadi ya maombi? Mungu anaweza kukuponya, kama utaamini. Huwezi kuketi hapo na kuishi, kama wale wenye ukoma walioketi langoni, wakasema, "Kwa nini tuketi hapa hata tufe?" Umewasiliana na *Kitu fulani*, unawasiliana Naye sasa. Uligusa vazi Lake, laiti ningaliweza tu kukufanya ulione! Unakufa kwa kansa, lakini kama utaamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakuponya.

243 Wale wenye ukoma walisema, "Kwa nini tuketi hapa hata tufe? Tukiketi hapa tutakufa." Ukiketi hapo, utakufa. Simama katika Jina la Yesu Kristo, nenda nyumbani ukaponywe basi.

244 Wote wanaotaka kumwamini Yeye, mnaamini kwa moyo wenu wote? Simameni kwa miguu yenu, kila mmoja wenu, na mkubali uponyaji wenu. Inueni mikono yenu. Haleluya!

245 Huyu—huyu hapa mwanamke mwingine kutoka kwenye kiti chake cha magurudumu akisimama. Wanasimama kila mahali, kote jengoni hapa chini, chini hapa ndani wanasimama. Simameni mtoke kwenye viti vyenu vya magurudumu, simameni. Hii ni. . .Mwana wa Mungu yuko miongoni mwenu,

Kristo Mponyaji. Simameni, inueni mikono yenu na mumpe Yeye sifa.

Bwana Yesu, ninamtoa pepo wa mashaka katika jengo hili.

Toka hapa, Shetani, ninakusai, katika Jina la Yesu Kristo.

61-0212E Ni Mimi Msiogope
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org